Maswali na Majibu Juu ya Roho Mtakatifu

Na baada ya usiku uliopita sisi sote tumejazwa. Nimesikia habari njema kuhusu wengi ambao wamepokea Roho Mtakatifu. Nasi tuna furahia hilo.

2 Tuna furaha kuwa na Ndugu Graham usiku huu, mmoja wa wasaidizi wetu hapa toka kwa maskani yale, mchungaji wa kanisa la utakatifu kule Utica. Na Ndugu Jackson, yeye alikuwa hapa usiku uliopita, naamini alikuwako; au yeye ako nyuma huku kwenye wasikizi mahali fulani sasa, mtu fulani alisema. Naam, namwona Ndugu Jackson nyuma kule kwenye wasikizi sasa. Na—na Ndugu Ruddell, je ako hapa usiku huu? Yeye ni mshiriki mwingine wetu nje hapa kwenye "62." Tuna furaha kuwa nao hapa. Na pamoja na . . . aha, Ndugu Pat, na ndugu hawa wengine, tuna—na kule nje kwenye wasikizi. Tuna furaha kuwa nanyi nyote hapa usiku huu.

3 Sasa, kama ningetaka kuhakikisha jambo hili, ningeleta baadhi ya wahubiri wazuri humu wawahubiri, kwa sababu nimepwewa na sauti kutokana na kuwa na wakati mzuri usiku uliopita.

4 Sasa, mke wangu, yeye ndiye anayenisahihisha, mwajua, ndugu, yale ninayonena. Yeye alisema watu kule nyuma usiku uliopita hawangenisikia, kwa sababu nilikuwa nikinena karibu sana na kitu hiki. Na sasa, kabla sijaanza, nitajaribu kitu fulani. Sasa, nashangaa kama hiki ni bora. Je, hiki ni bora kule nyuma? Au hiki ni bora? Je, hiki ni bora,? Sasa, mpenzi, huo ni wakati mmoja nina alama dhidi yako. Sasa, wanasema hicho ni bora. Vema. Jamani! Huyo ni mwanamke. Huyo ni mzuri, kwa sababu umekuwa wakati mrefu tangu nilipokuwa na moja. Yeye kila mara huwa sahihi.

5 Vema, bila shaka tulikuwa na—na wakati wa furaha kwa hizo ibada tatu za usiku; nilifurahiwa. Na sasa, kanda, zote isipokuwa za usiku uliopita . . . Nilimwita Ndugu Goad na kumwambia aje achukue kanda kwa ajili ya maskani. Lakini ikawa nilifahamu kuwa Billy Paul alichukua motokaa yake akaenda, kwa hivyo kanda hazikuchukuliwa kadiri nijuavyo. Kwa hivyo tuliukosa huo. Ningependa kuuweka kanisani kwa ajili ya kanisa kwa kuwa—mtu fulani asema—yale tunaamini.

6 Sasa, usiku huu nitanena kuhusu *Ule Mkutano Mkuu*, nikifaulu na kumaliza maswali kwa wakati. Ndiposa, kesho asubuhi ni ibada ya uponyaji. Nasi tutaombea wagonjwa. Kwa hivyo, hatuwezi kutoa—au kuendelea tu na kusema, "Sasa,

nitakuchukueni wewe na wewe, na wewe." Hilo halingekuwa sahihi. Lakini tunatoa kifurushi cha kadi, na mahali fulani katika kadi hizo, naita wachache jukwaani. Ndiposa, Roho Mtakatifu akianza kufunua, ndipo inapitia kwa wasikizi na kuwachukuwa watu katika wasikizi kwa ajili ya ibada ya uponyaji. Ndiposa, kesho asubuhi, nitanena, Bwana akipenda, kabla tu ya ibada ya uponyaji.

7 Namwona mke wangu akicheka. Mpenzi, huwezi kunisikia hata kidogo? Aha, unanisikia. Vema, hilo ni jema. Yeye huketi kule nyuma na kama ni—hawezi kunisikia yeye anatikisa kichwa chake, "Wewe . . . hatukusikii, hatukusikii."

8 Kwa hivyo basi kesho—kesho usiku ni ibada ya uijilisti pamoja na ibada ya ubatizo wa maji. Ndiposa, mara tu nimalizapo kuhubiri kesho usiku, tutafungua pazia na kuwa na ubatizo wa maji hapa kesho usiku. Bwana akipenda—Bwana akipenda, asubuhi nataka—au kesho usiku nataka kuongea kuhusu somo: *I—Ishara Ilitolewa*. Kisha kama tuko hapa Jumatano usiku, Bwana akinijalia kuwa hapa Jumatano usiku, nataka kuhubiri juu ya: *Tumeona Nyota Yake Mashariki Nasi Tumekuja Kumwabudu*. Sasa, hiyo ni hapa tu sikukuu ya Krismasi.

9 Ndiposa, mara tu baada ya Krismasi ni juma la likizo ya Krismasi. Hapo ndipo tuchukuapo barua zote . . . Ndugu Mercier na wengineo kila mara huzichukua zote, nasi huzitandaza zote, na kuziombea barua hizo na kumuuliza Bwana atuongoze ni wapi kote ulimwenguni tutakapoenda.

10 Sasa, Wafanyi Biashara Wakristo wana mlolongo mzima, huo ni kuwa Florida mara moja kwa mkutano wao. Niende toka pale hadi Kingston, kisha kule Haiti, na kushuka kwenda Puerto Rico, kuingia Amerika Kusini, kurudi kupitia Mexico.

11 Lakini yaonekana Bwana ananiongoza kwenda Norway. Sijui kwa nini. Mwajua kile kitabu kidogo kiitwacho *Mtu Aliyetumwa kutoka kwa Mungu?* Ndicho nakala ya kidini itolewayo sana nchini Norway. Wazia hilo, yale Bwana ametenda kule. Na nilipokuwa kule, hawangeniruhusu niweke mikono juu ya wagonjwa. Nilikuwa kule usiku mtatu. Nao hawangenikubalia niweke mikono juu ya wagonjwa. Kwa hivyo mwaona yale Mungu anaweza kufanya. Umati wa watu ulikuwa mkubwa sana iliwabidi wachukue askari wanaotumia farasi, farasi, kuwaondoa watu kwenye njia za mji ili nifike mahali pale. Na sikuweka mikono juu ya wagonjwa. Ingawaje, niliwaombea; na kuwaambia wawekeane mikono wao kwa wao.

12 Kwa hivyo . . . [Ndugu Branham aongea na mtu fulani—Mh.] Sasa kesho asubuhi . . . Sasa, usiku huu, labda tutaendea maswali haya, kwa sababu tunayo mazuri sana. Nami sijui ni muda gani Bwana atatukawisha kwa kwayo. Ndiposa, kesho asubuhi Billy Paul, au Gene, au Leo, mmojawao, atakuwa hapa

kutoa kadi za wanaohitaji maombi saa 2:00 hadi saa 2:30. Sasa, watu wanaotoka nje ya mji, hebu niwakumbushe tena msisahau. Kama mngependa kuingia msarini, ni heri tuwachukue watokao nje ya mji huu ikiwezekana.

13 Sasa, wakati mwingine hapa kanisani sisi hufikia mahali ambapo wao husema, "Vema . . . " Tunawachukua watu watokao nje ya mji, tukawaleta . . . Mtu fulani atasema, "Vema, sijui imekuwaje kwao. Huenda wamekuwa wakimwambia uongo." Kisha unakuta watu mjini; wao husema, "Ee, huenda ulisha wajua." Kwa hivyo . . . Ndipo wao husema—imesemwa, "Vema, nitawaambia, ni kadi za maombi." Vema, na wale wale wasio na kadi za kuombewa, je? Na kumekuwa siku baada ya siku wakati ni . . .

Wasemaje? [Ndugu Branham anaulizwa arudi nyuma kidogo toka kwa maikrofoni—Mh.] Nisonge nyuma ya maikrofoni? Vema, mwajua, mimi kila mara huhubiri katikati ya njia. Kwa hivyo labda ningeichukua tu hivyo. Hivyo ni bora? Hivyo ni bora. Ni vema. Nitawaambia ni nini. Maikrofoni ze—zetu ni duni mno hapa, duni mno. Nasi hatujaribu kuzirekebisha hata kidogo sasa, kwa sababu tunataka maskani mapya yajengwe mara moja. Na ndipo tutakapokuwa na nafsi nyingi sana (ona?) kama tunaweza kuja hapa na kupanua mahali hapa pawe pakubwa kidogo na kujenga vyumba vingine zaidi, na tujitayarishe kwa mikutano tunapokuwa nayo hapa.

14 Na sasa, kumbukeni, asubuhi vijana, mmoja au watatu wao watakuwa wakitoa kadi kati ya saa 2:00— au 2:30 na 2:00. Hilo litampa kila mtu nafasi ya kutulia. Nami nilikuwa nikieleza jinsi wanavyosambasa kadi, sababu gani sisi huzisambasa. Ni kuweka utaratibu, Ona? Sasa, vipi kama ningalikuja humu, hivi sasa tu na kusema, "Hebu mwanamke *huyu*, mwanamke *huyu*, na mwanamume *huyo*, na mwanamke *huyu* . . . ?" Mwaona, hilo lingekuwa—hilo lingekuwa gumu. Ona? Ndiposa, kama wewe una . . . Wakati mwingi nimefanya hili. Na kama hawako wengi sana asubuhi, huenda nikafanya vivyo hivyo. Nitasema, "Watu wangapi ndani humu wanatoka nje ya mji walio na shida fulani, simameni."

15 Ndugu Mercier, utakuja kunisaidia. Utanisaidia? [Ndugu Mercier ajibu—Mh.] Ee, utakuja . . . Anakuja kwa kasaidiwe mwenyewe. Niliongea na mpenzi wako leo. Sasa, heri uwe mwema sana kwangu. Ona? Vema. Hilo ni nzuri. Ni—napenda ujasiri huo Ndugu Leo. Lisipokuwa sahihi, hebu—hebu tulisahihishe vema kadiri tuwezavyo, vema tuwezavyo.

16 Kwa hivyo sasa basi huuliza tu watu watokao nje ya mji huu wainue mikono yao walio na shida. Na ndipo nasimama tu pale, nashughulikia mtu mmoja hata Roho Mtakatifu aanze, na kuchukuwa wasikizi wote. Wangapi wamekuwa humu na kuona

hilo likitendeka ndani humu? Hakika! Ona, ona? Kwa hivyo haijalishi ni njia gani inayotamiwa. Ni . . .

17 Nawatakeni mkumbukeni hili, nami nitajaribu kulieleza asubuhi tena. Mataifa, Injili waliyopewa ni Injili ya imani, si ya kazi kamwe. Ona? Na kama nilivyosema usiku uliopita. Roho Mtakatifu aliposhuka katika Pentekoste, walipowaendea Wayahudi (Matendo 19:5), iliwabidi wawawekee mikono juu yao ili wampokee. Na walipoenda kwa Wasamaria, iliwabidi kuwawekea mikono. Lakini walipowajia Mataifa nyumbani mwa Kornelio, "Hata Petro alipokuwa akinena maneno haya . . . " Hamna kuwekeana mikono.

18 Yule msichana mdogo alipokufa, binti Yairo, yule kuhani, kasema, "Njoo uweke mikono juu yake, naye ataishi." Lakini yule akida wa Kirumi, Mtaifa, alisema, "Mimi sistahili Wewe uingie chini ya dari yangu, sema neno tu." Naam. Mwaona?

19 Yule mwanamke Msirofoinike, hasa yeye alikuwa Myunani, wakati yeye—wakati Yesu alipomwambia, kasema, "Si vema kukitwaa chakula cha watoto na kukitupitia mbwa."

Yeye alisema, "Kweli Bwana: lakini mbwa chini ya meza hula makombo ya watoto."

Yeye alisema, "Kwa sababu ya neno hilo, pepo amemtoka binti yako." Sema mambo mazuri basi. Sema jambo nzuri kuhusu mtu fulani. Ongea kuhusu Yesu. Nena jambo jema, jambo halisi. Hiyo ndiyo njia ya kuwaondosha pepo. Yeye hakusema kamwe—Yeye hakuombea msichana huyo. Yeye hakusema jambo moja kuhusu kuponywa kwa msichana huyo. Yeye alisema tu, "Kwa sababu ya neno hilo, kwa sababu ya neno hilo . . . "

20 Hattie Wright, hivi majuzi, hakuomba lo lote. Alikuwa tu ameketi pale lakini alinena neno linalofaa, lililompendeza Roho Mtakatifu. Na Roho Mtakatifu akajibu na kusema, "Hattie, omba lo lote upendalo, lo lote uhitajilo na utakalo. Tazama kama hii ni halisi ama sivyo. Omba lo lote (kuponywa kwa dada yake mdogo aliyelemea aliyeketi pale amelemea kabisa, dolla elfu kumi ili asilime milimani mle; ujana urudishwe kwa mwili wake uliodhoofika); cho chote unachotaka kuomba, uliza hivi sasa. Kama hatashuka na kukupa hivi sasa, basi mimi ni nabii wa uongo." Hilo ni—hilo ni—hilo ni jambo kubwa, sivyo?

21 Yesu alisema, "Uambie mlima huu . . . " Na mmesikia ku—kuhusu yale—yale yamekuwa yakitendeka; hiyo ndiyo huduma tunayoingia. Tuko mbali njiani sasa. Hivi punde Bwana Yesu atakuja. Nasi yatubidi tuwe na imani ya kunyakuliwa Kanisani ambapo twaweza kugeuzwa katika kufumba na kufumbua macho kuondoka, la sivyo, hatutanyakuliwa. Lakini msijali, itakuweko. Itakuweko. Na nguvu za *kanisa* hili zitakapoongezeka, litaleta ndugu zake; nguvu za *kanisa* hilo ziongezeke, zilete ndugu zake; nguvu za *kanisa* hilo zitaleta

ndugu wengine; kisha kutakuwako na ufufuo wa wote. Nasi tunatazamia hilo.

22 Sasa, msisahau, kadi za maombi asubuhi saa 2 mpaka saa 2:30. Ndipo nawauliza zo zote zilizokuwamo, ndipo waache kutoa kadi, warudi, na kuketi (ona?) kwa sababu labda watakuwa wamesha toa zote wakati huo haidhuru, au kadiri tutakazoweza kuleta toka pale mahali fulani. Hao wavulana wataamka, wachanganye kadi zote mbele zenu, ndipo ukitaka moja, unataka moja, au cho chote kile . . . Kisha nijapo, nita . . . Po pote Bwana asemayo nianzie kuitania . . . Na kama Yeye akisema, "Usiite yo yote." Sitaziita kamwe (Ona?), lo lote lile.

23 Nami . . . Huduma hiyo karibu tu inafifia haidhuru; kuna kitu fulani kikubwa kinachokuja. Kumbuka, hapo ndipo kila wakati imesemwa kote katika jukwaa hili au kote mimbarani hapa, na bado halijakosa kutimia. Mwakumbuka huduma ile ya kutumia mkono? Mwaona kile ilifanya? Mawazo ya mioyo, mwaona kile ilitenda? Sasa tazama hili: nena Neno, uone yale yanatendeka. Ona? Niliwaambia ninyi hapa miaka mingi iliyopita—kanisa hili (naongea na maskani haya)—miaka mingi iliyopita, miaka mitatu ama minne iliyopita, jambo fulani lingetendeka. Linakaribia kutendeka. Na hapa sasa inaonekana tu moja kwa moja kwa . . . Linajiandaa. Sasa, tuna shukrani kwa hilo. Lo, tuna shukrani jinsi gani. Tuna furaha sana.

24 Sasa, tuna maswali magumu sana hapa, nasi tunataka kuyaendea. Mtu fulani alitazama vitabu hivi vyote nilivyokuwa navyo. Nilisema, "Vema, mtu mwerevu huhitaji kimoja tu." Lakini mimi si mtu mwerevu. Yanibidi niwe na vingi sana vya kuchunguzia. Vema, hii ni *Diaglott*, na hii ni Biblia, na hii ni kamusi. Kwa hivyo ni . . . Tutamuuliza tu Bwana atusaidie sisi na kutuongoza kujibu maswali haya kulingana na mapenzi Yake ya Kiungu pamoja na Neno Lake.

25 Kwa hivyo sasa, hebu sasa tuinamishe vichwa vyetu kwa dakika chache kwa maombi. Bwana, tuna shukrani kwako toka kilindi cha mioyo yetu kwa ajili ya yale Wewe umetufanyia katika huu usiku mtatu uliopita. Ee, kuona wahudumu wakikutana nyuma kule chumbani na kusalimiana kwa mkono na kwa imani iliyoimarishwa, —na—na kuchukua hatua mpya. Wakipiga simu . . . Na mioyo yetu ikifurahi, na watu wakimpokea Roho Mtakatifu baada ya wao kuwa—kuona Neno Lako, jinsi laeleza hasa hatua kwa hatua jinsi ya kupokea Roho Mtakatifu Wako. Tuna shukrani sana kwa hilo, Bwana.

26 Unaturahisisishia sana mambo, kwa sababu sisi tu watu vivi hivi. Nasi twaomba, Mungu, kuwa—kuwa utatuwezesha kujinyenyenyekeza kabisa daima, kwa maana ni . . . Ni hao wanaojidhili ambao watakwezwa. Na hekima ya ulimwengu huu ni upumbavu kwa Mungu; Mungu alipenda kuwaokoa wale waliopotea kwa upuzi wa lile Neno linalohubiriwa.

27 Na sasa, Baba, hapa nina maswali kadha yaliyoulizwa kwa mioyo minyofu inayohusika. Na moja walo likijibiwa kwa kosa huenda laweza kumtupili mtu huyo makosani, kutoa nuru baya kwa swali lao linalowatatiza. Kwa hivyo Bwana Mungu, naomba kuwa Roho Mtakatifu ataenea juu yetu sisi na atatufunulia mambo haya, maana imeandikwa Maandikoni, "Ombeni nanyi mtapokea; na tafuteni—nanyi mtapata; bisheni nanyi mtafunguliwa." Na hilo ndilo tunalofanya sasa, Bwana, kubisha mlangoni Pako pa neema. Tukisimama katika uvuli wa haki Yako Takatifu, tunaomba sana Damu ya Kristo wa Mungu na Roho Matakatifu.

28 Nasi hatuji usiku huu tu kwa sababu eti tumemaliza usiku huo mtatu mahubiri kuhusu Roho Mtakatifu, tunakuja kwa unyenyekevu sana na uaminifu. Tunakuja hivyo kama kwamba huu ulikuwa usiku wa mwisho tutakaowahi kuwa duniani. Tunakuja tukiamini kuwa utajibu maombi yetu. Na Bwana, twakuomba wewe sasa kututosheleza kwa Uzima Wako wa Milele. Na katika kujibu Neno Lako, na Roho Mtakatifu. . . Ee Mungu, kama tulivyoona kwamba ni Wewe Mwenyewe kati yetu, twaomba kuwa Yeye atatufunulia sisi usiku huu mambo ambayo tunayohitaji. Nasi twaomba tu kuwa nafsi zetu zitatulia, na mawazo yetu yawe na amani na kuwa na imani katika Mungu tupate kusonga mbele kudai baraka ambazo Yeye aliahidi. Twaomba katika Jina la Yesu. Amina.

29 Sasa, ninayo maswali yote niliyopewa, isipokuwa moja. Nami nilimjibu maskini Ndugu Martin, aliyeniuliza swali usiku wa juzi, moja pekee. Kulikuwako mengi hapa usiku uliopita, lakini yalikuwa ya haja za maombi. Na Ndugu Martin aliniuliza swali kuhusu Yohana 3:16—au Yohana 3, naamini, kuhusu, "Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuona Ufalme," na kuilinganisha na ukanda niliokuwa nimetoa wa Waebrania. Nami nilimkuta katika chumba cha nyuma kule jioni iliyopita, na—kabla sijapata nafasi ya kumjibu, ndiposa nikafanya hivyo kule, kuhusu somo lile.

30 Sasa, kuna mtu ye yote ambaye hakuwako hapa usiku uliopita, hebu tuone mikono yenu, ambao hawakuwa hapa usiku uliopita. Loo, laiti mngelikuwa pamoja nasi. Tulikuwa na wakati wenye fahari, Roho Mtakatifu . . .

31 Huenda, kwa dakika moja tu. . .Halitadhuru. Huu unanaswa ukandani. Na mhudumu ye yete asipo—au mtu ye yote asipokubaliana na yale nitakayonena sasa, au hata katika maswali, naomba, ndugu, kuwa hutayaona mageni, lakini kwamba—kumbuka kuwa kanda hii inanaswa maskanini mwetu hapa. Tunawafundisha watu wetu. Wahudumu wengi wa imani mbali mbali wameketi hapa. Nami ningependa kuingilia somo lile tena, kwa kuwa kunao baadhi ya watu wetu ambao hawakuweza kuhudhuria usiku uliopita ambao nawaona humu usiku huu. Nami ningependa kurudia hayo kidogo, mkiniruhusu,

yale niliyonena jioni iliyopita; na hilo lilihusu Pentekoste, kuhusu kumpokea Roho Mtakatifu.

Sasa, tukisoma *Emphatic Diaglott* ya Kiyunani, niliposoma jioni iliyopita, ambayo ni wazi mbele yangu sasa. Hiyo ndiyo tafsiri ya asili toka kwa Kiyunani hadi kwa Kiingereza. Haipitii kwa wafasiri wengine, ni—na tafsiri zingine, ni moja kwa moja toka katika Kiyunani hadi kwa Kiingereza. Sasa, maneno ya Kiingereza, wakati mwingi yana maana mbalimbali, kama vile ningelisema sasa, *board* (halmashauri). Chukua neno hilo board. Ungesema, "Vema, yeye alimaanisha *boring him* (kumchosha)" La! "Yeye—yeye alilipa *board* (nauli) yake." La! Vema, yeye. . . "Ni *board* (ubao) kwenye ukuta wa nyumba." Vema, ona? Au yo yote ya hayo. . .Kuna maneno manne ama matano mbalimbali yangelitumiwa; yakubidi upate sentensi hiyo. Neno *see*. *See* maana yake ni "kufahamu," katika Kiingereza. *Sea* maana yake ni "ziwa." *See* maana yake ni "kutazama." Ona? Lakini kwenye tafsiri hizi, neno lililotumiwa hapa, nililonena usiku uliopita katika Matendo sura ya 2, ambapo yasema, "Ndimi za moto zikawakalia. . . " Sasa, ningependa kurudi nyuma kidogo. Je, mngependa, kwa dakika chache, tukayarudie kidogo kabla hatujaendelea mbele?

32 Sasa, fungua, katika tafsiri zenu za King James au tafsiri yo yote unayosoma. . .Nami nataka kuisoma. Na sikizeni kwa makini sasa. Msifahamu kwa kosa. Wengi leo, hata dada yangu, wengi wao walipiga simu kasema. . .Bi Morgan. . .Wengi wao walikuwemo jioni iliyopita. Bi Morgan ni mmoja wa dada zetu hapa aliyekatiwa tamaa; naye alikuwa kwa orodha ya wanaokufa katika Louisville kwa miaka kumi na sita au kumi na saba iliyopita akiwa na ugonjwa wa kansa. Nadhani yeye anaketi nyuma hapa tena usiku huu. Yeye hangesikia, alisema, kwa sababu nilikuwa naongea karibu sana na maikrofoni. Na kwa ajili yao nataka kurudia hili kwa dakika chache.

33 Sasa ninasoma katika Andiko hili la Matendo 2.

> . . .*ilipotimia siku ya Pentekoste walikuwako wote* katika nia *moja*.

Naam, napenda hilo sana kuliko "moyo mmoja," maana, mnaweza katika moyo mmoja katika karibu kila jambo, bali hapa nia zao zilikuwa pamoja.

> . . .nia *moja, na mahali pamoja*.
>
> *Kukaja ghafula toka mbinguni, uvumi* kama upepo mkali sana ukienda kasi*, ukaijaza nyumba* yote *waliyokuwa wameketi*. (si kupiga magoti, si kuomba; bali kuketi.)
>
> Ndimi zilizogawanyikana, (n—d—i—m—i—) *ndimi "zilizogawanyikana"* maana yake ni ndimi "zilizogawanyikana" zikawatokea, kama moto, na mmoja ("mmoja", umoja.) ukawakalia *kila* mmoja *wao*.

> Kisha wote wakajazwa, ("kisha", kiunganisho), *wote wakajazwa* Roho *Mtakatifu, wakaanza kusema kwa lugha nyingine, kama Roho alivyowajalia kutamka.*
>
> *Sasa walikuwako* katika *Yerusalemu Wayahudi Watu, watauwa, watu wa kila taifa chini ya mbingu.*
>
> Wakati hii, basi repoti hii ikisha enezwa, *makutano walikutanika, wakashikwa na fadhaa, kwa kuwa . . . kila* mmoja alimsikia akisema *kwa lugha yake mwenyewe.*

34 Sasa tazama! Moto ulipokuja, ulikuwa ndimi; walipokua wakinena, ilikuwa lugha. Sasa, kuna tofauti kubwa kati ya ndimi na lugha. Kwetu ni sawa. Lakini katika Kiyunani *"ndimi"* maana yake ni *huu* [Ndugu Branham aonyesha—Mh.] sikio, *hili*. Ona? Huo haumaanishi lugha: huo unamaanisha sehemu ya mwili inayoitwa ulimi. Ukichunguza, imetafsiriwa *ndimi za moto* ambayo maana yake ni "kama ndimi," kama tu lambo la moto, mwali mrefu wa moto. Sasa, tazama huo mkazo sasa. Na kila mojawapo wa mahali hapo sasa, usiisahau.

35 Sasa, tutaonyesha mchezo mdogo wa kuigiza usiku huu. Na nitaiacha juu yenu. Sasa kumbuka, kama kitu cho chote ni kinyume, hilo ni juu yako. Lakini njia pekee ambayo mtu ye yote aweza kupata cho chote toka kwa Mungu ni kwa imani. Na kabla hujaweza . . .

36 Yanibidi kujua kile ninachotenda kabla sijakuwa na imani katika kile ninachotenda. Mbona ukamwoa mke wako? Ulikuwa na imani kwake. Uliisha mjaribu, ukamchunguza, ukaona alikotoka, alivyokuwa. Hivyo ndivyo yalivyo Maandiko na Mungu pia. Hilo ndilo linalosababisha maono haya, ile—hii Nguzo ya Moto, mambo haya yote, kwa sababu Mungu aliyaahidi. Mungu alisema hivyo. Nimemjaribu kwa Neno Lake na kujua kuwa ni Kweli. Nanyi fuateni Neno Lake. Ndipo kama kuna tatanisho ndogo mahali fulani, basi kuna kasoro mahali fulani. Kwa maana Mungu (sikiza!)—Mungu hakufanya kamwe au hatafanya kamwe kinyume au kinyume cha kanuni Zake. Majira ya baridi hayatakuja katika majira ya joto, na majira ya joto hayatakuja katika majira ya baridi. Majani hayatapukutika katika majira ya kuota na yaote katika majira ya kupukutika. Haiwezekani kamwe.

37 Kama nilivyosema usiku uliopita kuhusu chemchemi, inayonyunyizia mimea yako. Au kama unasimama nje hapa katikati ya shamba, na ni giza kabisa, nawe ungesema, "Ee, stima kuu, najua uko uwandani. Sasa, nimepotea, sijui ninakoenda. Angaza, ili nione jinsi ya kutembea! Kuna stima ya kutosha kuangazia uwanda mzima." Hiyo ni kweli. Naam, bwana! Kunayo stima ya kutosha chumbani humu kuangazia hata bila taa, bila hiyo. Lakini yakubidi uiongoze. Sasa, huenda ukaipigia makelele hadi usiweze kupiga makelele tena,

haingewaka. Lakini ukifanya kazi kulingana na kanuni za stima, basi utapata mwangaza.

38 Vema, hivyo ndivyo ilivyo kwa Mungu. Mungu ni Muumba mkuu wa mbingu na nchi, Yeye yule jana, leo, na hata milele. Yeye yuangali Mungu. Lakini Yeye hutenda tu ukifuata kanuni Zake na maagizo. Marafiki, nasema hili: Sijaliona likishindwa kamwe, na haitashindwa.

39 Sasa, hebu tuchunguze. Yesu katika Luka 24:49 alikuwa amewaagiza mitume baada ya wao kuokolewa na kutakaswa kulingana na Neno; kuhesabiwa haki kwa kumwamini Bwana Yesu; kutakaswa katika kwa Yohana 17:17 Yesu aliposema, "Uwatakase, Baba, na Kweli. Neno Lako ni Kweli." Na Yeye alikuwa Neno.

40 Sasa, akawapa nguvu za kuponya wagonjwa, kutoa pepo, kuwafufua wafu; nao wakarudi wakifurahi. Na majina yao yalikuwa kwenye kile Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo. Mwakumbuka jinsi tumeeleza hayo sasa. Lakini hawakuwa wameongoka bado. Yesu alimwambia Petro usiku wa kusulubiwa Kwake; akasema, "Nawe utakapoongoka, waimarishe ndugu zako."

41 Roho Mtakatifu ni kile . . . Unaamini hata Uzima wa Milele, lakini Roho Mtakatifu ajapo ni Uzima wa Milele. Unaamini . . . Wewe unazaliwa kwa Roho unapotakaswa, lakini hujazaliwa na Roho hata Roho Mtakatifu akuingie. Hilo ni kweli. Mtoto ana uzima tumboni mwa mama, misuli midogo inatapatapa; ni uhai fulani. Lakini ni uhai tofauti anapopumua pumzi ya uzima mapuani mwake. Ni tofauti. Hivyo ndivyo ilivyo, ni . . .

42 Ndugu yangu mpendwa Mmethodisti, na Pilgrim Holiness, na Nazarini, ubatizo wa Roho Mtakatifu ni tofauti na utakaso. Utakaso ni kusafishwa, ambako ni matayarisho ya uzima. Lakini Roho Mtakatifu ajapo, ni Uzima. Matayarisho ni kusafishwa kwa hicho chombo; Roho Mtakatifu ni kukijaza hicho chombo. *Utakaso* maana yake ni "kusafishwa na kutengwa kwa ajili ya matumizi." Roho Mtakatifu ni kukitumikiza. Wewe u chombo ambacho Mungu amekisafisha.

43 Nasi twaona kuwa Roho Mtakatifu ni Mungu Mwenyewe ndani yako. Mungu alikuwa juu yako katika ile Nguzo ya Moto pamoja na Musa. Mungu alikuwa pamoja nawe katika Yesu Kristo. Sasa Mungu ako ndani yako katika Roho Mtakatifu. Si miungu mitatu, Mungu mmoja akitenda kazi katika afisi tatu.

44 Mungu akijinyenyekeza, akishuka toka juu ya mwanadamu. Yeye hangemgusa, kwa sababu yeye alikuwa ametenda dhambi katika bustani ya Edeni na kujitenga mwenyewe na ushirika Wake. Ndipo nini ilitendeka? Yeye ilimbidi awe juu yake. Damu ya fahali na mbuzi haingemruhusu Yeye kushiriki na mwanadamu tena; lakini kupitia kwa torati na maagizo, ikionyesha kimbele wakati huu unaokuja, wa kutoa sadaka ya

fahali, na kadhalika, na kondoo…Ndipo Mungu aliposhuka na kukaa katika mwili uliotakasika, akazaliwa na mwanamke bikira, ambapo Mungu Mwenyewe…Wajua kile Mungu alifanya? Yeye—Yeye hakufanya lo lote ila tu…Yeye alipiga Hema Lake kwetu. Mungu aliishi katika Hema lililoitwa Yesu Kristo. Yeye alipiga tu Hema Lake pamoja nasi, akawa… (Nita—nitahubiri hilo asubuhi, kwa hivyo heri niliache pekee.) Sasa, hilo—jinsi Mungu alipiga hema—au akakaa kwetu.

45 Na sasa Mungu yuko ndani yetu. Yesu alisema katika Yohana 14, "Siku hiyo mtajua kuwa Mimi niko ndani ya Baba, Baba ndani Yangu, Nami ndani yenu, nanyi ndani Yangu." Mungu ndani yetu. Kusudi Lake lilikuwa nini? Kutekeleza mpango Wake.

46 Mungu alikuwa na mpango. Yeye alitaka kufanya kazi kati ya binadamu, basi akaja katika ile Nguzo ya Moto, ambao ulikuwa Moto wa kisiri ulioning'inia juu ya wana wa Israeli. Kisha Moto huo ukadhihirishwa katika mwili wa Yesu. Naye alisema Yeye alikuwa moto huo. "Ibrahimu asijakuwepo MIMI NIKO." Yeye alikuwa huo moto. Yeye alisema, "Nalitoka kwa Mungu, nami narudi kwa Mungu." Na baada ya kifo Chake, kuzikwa, na kufufuka, Mt. Paulo alikutana naye njiani—wakati jina lake lilikuwa lingali Sauli—njiani akienda Dameski, na Yeye alikuwa amegeuka tena kuwa hiyo Nguzo ya Moto. Nuru ikampofusha macho. Naam.

47 Na Yeye yuko hapa leo, Nguzo ya Moto ile ile, Mungu yule yule akifanya ishara zile zile, kazi zile zile. Kwani? Yeye anafanya kazi kati ya watu Wake. Yeye yuko ndani yetu. Ni…Yeye yuko pamoja nanyi sasa, "lakini nitakuwa ndani yenu. Nitakuwa pamoja nanyi hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari," ule mwisho wa ulimwengu. Yeye atakuwa pamoja nasi.

48 Sasa, tazama. Yesu alikuwa amewaagiza waende Yerusalemu na kungoja. Neno *kaeni* maana yake ni "kungoja," halimaanishi kuomba, lamaanisha "kungoja." Hawakuwa raia waliofaa kwa kuhubiri, kwa sababu walijua tu kufufuka kwa Utu Wake, kwa kumwona kwa mwili tu. Yeye—Yeye aliwaamuru wasihubiri tena, wasifanye lo lote mpaka kwanza wamepata Uwezo utokao juu.

Siamini kuwa mhubiri ye yote ametumwa na Mungu au aweza kuwekwa mikono sahihi…Kwa sababu Mungu hana kikomo. Na yale Mungu afanyayo mara ya kwanza, Yeye huyafanya hayo wakati wote. Sasa, kama Mungu hangewaruhusu hao kuhubiri mpaka walipopita kwa Pentekoste na kupokea ujuzi wa Pentekoste, hamna mtu, isipokuwa ameagizwa na hamu au ameagizwa na dhehebu fulani, ana haki ya kuingia mimbarani mpaka amejazwa na Roho Mtakatifu. Hiyo ni kweli hasa. Kwa sababu yeye anawaongoza kwa maarifa ya kielimu ya dhehebu fulani mpaka amejazwa na

Roho Mtakatifu; ndiposa, yeye anawapa wao chakula cha hua; *Mwana-Kondoo Pamoja na Hua*, kama tulivyonena usiku uliopita.

49 Sasa tazama. Yeye alisema, "Enendeni Yerusalemu mkakae pale; ngojeni tu mpaka nitakapowatumieni ahadi Yake Baba." Na ndipo, wao walifanyaje? Wao walikuwa watu mia na ishirini, wanaume kwa wanawake. Walienda katika chumba cha juu mle hekaluni.

Sasa, ilikuwa inakaribia ile siku ya Karamu ya Pentekoste, tangu kusafishwa kwa madhabahu, kule kuchinjwa kwa yule mwana-kondoo wa pasaka mpaka kule—kule kuja kwa Pentekoste, ambako kulikuwa ni malimbuko, sikukuu, sikukuu ya Pentekoste. Na kwenye majengo yale . . .

50 Sasa, nimekuwa katika nchi hizo. Nchi za mashariki hazikuwa na ngazi upande wa ndani. Ngazi zilikuwa nje. Nje ya hekalu, tumeambiwa, kulikuwa na ngazi zilizoelekeza kwenye chumba kidogo mle; kupanda juu, juu, juu, hadi ufikie juu kwenye chumba kidogo mle, kama ghala juu ya hekalu, chumba kidogo, orofani. Na Biblia ilisema kuwa wao walikuwa ndani mle na milango ilikuwa imefungwa, kwa sababu wao walikuwa wanawaogopa Wayahudi, kwa sababu wangewaangamiza kwa kumwabudu Bwana Yesu, baada ya kuhani mkuu Kayafa, na Pontio Pilato, na wengineo kumuua Yeye. Kwa hivyo wao wangewangamiza wote wajiitao Wakristo. Na milango ilikuwa imefungwa, nao walikuwa wakingoja.

51 Sasa, katika vyumba kama hivyo, hamna madirisha. Madirisha yalikuwa vifito kama milango, vilifunguliwa kwa kuvutwa. Katika vyumba hivyo kuna taa ndogo za mafuta zilizoning'inia chini na kuwaka . . . Ukiwahi kuwa California kwenye Mkahawa wa Clifton, enda kwenye orofa ya chini, na utapata mojwapo wa aina kama hizo, kwenye orafa. Mmewahi kuwa kule? Wangapi ndani humu wamekuwemo mle? Nawaona watu wakiitikia kwa vichwa vyao. Vema, mwajua ninayonena. Vema. Enda chini pale, na utaona Bustani ya Gethsemane; kabla kuifikia, utapitia katika mojawapo wa hivyo vyumba vya kimashariki. Ndivyo hasa. Pale utapata taa ndogo iliyojaa mafuta ya mzeituni pamoja na utambi mdogo wa sufu ndani yake, ikiwaka."

52 Sasa, hebu tuseme walikuwa juu pale, wakipanda upande huu wa nje. Wakafika juu pale na kujificha, kwa sababu waliwaogopa Wayahudi. Yesu hakuwaambia waende orofani. Yeye alisema, "Kaeni Yerusalemu." Kama walikuwa chini hapa katika nyumba, ni vigumu kutambua kipi kitatendeka. Wangeingia na kuwakuta. Kwa hivyo walienda kwenye chumba kidogo kikuukuu pale orafani, pale juu kwenye orofa ya juu kabisa, nao wakafunga chumba kile ili Wayahudi wale wasiingie waliko. Nao waliketi pale siku kumi wakingoja.

53 Sasa, sasa, tuko katika Matendo 1. Sasa, sikiza kwa makini sasa. Mnafahamu? Nje ya jengo zile ngazi zilielekea juu, nao waliingia katika hiki chumba kidogo. Chini pale hekaluni walikuwa wana ile Karamu ya Pentekoste. Ee, kulikuwa na furaha tele. Sasa, siku ya Pentekoste ilipotimia, wote walikuwa na moyo mmoja, moyo mmoja, wakiamini kuwa Mungu atatuma ahadi hiyo. Na kila mtu ndani humu awe katika nia hiyo usiku huu na aone kipi kitatendeka. Haina budi kujirudia. Ni ahadi kama tu ile waliyokuwa nayo. Ona?

54 Wao walikuwa wakifanya nini? Wakifuata maagizo, wakifuata zi—zi—zile sheria za Mungu: "Ngojeni mpaka . . . "

55 Sasa, wao waliwaogopa Wayahudi. Sasa, kumbuka hilo. Waliwaogopa Wayahudi. Basi, kwa ghafula kukaja uvumi kama uvumi wa upepo wenye nguvu ukienda kasi. Haukuwa upepo unaovuma; ilikuwa kama upepo unaovuma. Nitasoma maelezo haya katika dakika chache ya mfasiri. Ilikuwa kama uvumi wa upepo. Yaani, ulikuwa upepo wa kimbinguni (loo!), kitu ambacho wangesikia. Upepo huo ulikuwa ndani yao. Kukaja u—uvumi kama uvumi wa upepo. Upepo huo haukuwa ukivuma, lakini ulisikika tu kama uvumi wa upepo, kama kitu fulani kikisema [Ndugu Branham afanya sauti ya upepo—Mh.] Je, mmepata kuusikia? Lo! Kama uvumi wa upepo. Sasa tazama. Nao ulijaza . . . Sasa, ndani hapa ilisema, "wote," lakini katika Kiyunani ilisema "yote (y-o-t-e)—Nyumba yote," kila mahali ndani mle. Kila ufa, pembeni, na mwanya palionekana pamejawa nao. Si kusema, "Aisee, ndugu, je, mnajisikia ninavyojisikia?" La! Ulijaa kote, kama upepo unaovuma. Sasa tazama. "Kukaja uvumi kama uvumi wa upepo wa nguvu ukienda kasi na (kiunganisho. Sasa tazama hizo "na." Ona?) Usipozitazama, utaifanya iseme kitu fulani ambacho haisemi. Ona?)—na kama (kitu cha kwanza kutendeka kilikuwa sauti, kitu kama upepo ulioenda kasi ukawajilia)—na (mnakumbuka, usiku uliopita nilienda kwenye duka la kuuzia mboga nikanunua mkate na nyama. Hicho ni kitu kilichoandamana nao. Mkate ni kitu kimoja, nyama ni kingine. Na sauti ilikuwa kitu kimoja kilichowagusa)—na ukawatokea, (mbele zao) ndimi—ndimi zilizogawanyikana."

56 Je, kunaye ye yote humu aliyewahi kuona sinema ya *Amri Kumi* ya Cecil De Mille? Je mliona wakati zile Amri zilikuwa zikiandikwa? Jinsi yeye alivyolipata, sijui. Kulikuwako vitu viwili au vitatu nilivyoviona ndani yake nikavipenda sana. Jambo la kwanza ni hiyo nuru ya zumaradi, hivyo ndivyo hasa hiyo inavyoonekana. Ona? Jambo jingine lilikuwa wakati zile Amri kumi zilipoandikwa, na ilipomarizika, mliona hizo ndimi ndogo za moto zilitoka kwenye hiyo Nguzo kuu ya Moto? Je, mlitambua hilo? Sasa, hivyo ndivyo nadhani ilikuwa siku ya Pentekoste. Kukawatokea . . . Kwa hivyo wao wangeziona. Haikusema, "Zilianguka ndani yao." Lakini kukawatokea ndimi

(tutaziita), ndimi, kama ndimi ulimi huu hapa, [Ndugu Branham aonyesha—Mh.] umbo la ulimi, ulimi wa moto. Sasa, sikio—kama nilivyosema, sikio ni sikio; kidole ni kidole. Kidole hakimaanishi ulikisikia; inamaanisha ilionekana kama kidoleo. Na kama ingalikuwa sikio, haimaanishi walisikia, ilionekna kama sikio. Huu ulikuwa moto uliofanana na ulimi, si mtu fulani akiongea, moto uliofanana na ulimi.

57 Sasa hebu tuone jinsi Kiyunani kinavyosema hapa.

> Kukaja ghafula uvumi . . . kama *upepo wa nguvu ukienda kasi . . .*

> *(Ya 3, aya ya 3.) Kisha ndimi zilizogawanyika zikawatokea . . .*

Si kwamba ndimi zilizogawanyikana zilikuwa *ndani* yao, ama kwamba walikuwa *wakinena* na ndimi zilizogawanyikana. Ilikuwa, "Ndimi zilizogawanyikana ziliwatokea." Sasa, tazama. Haziko juu yao babo. Zimo mle chumbani, zikizunguka-zunguka kila mahali-kama katika upepo huu.

. . . zikawatokea, kama moto. Ndimi zilizogawanyikana zikawatokea (hiyo ni, *mbele* zao), kama moto (ndimi kama moto), *kisha* mmoja (umoja) ukamkalia *kila* mmoja *wao*. Si eti zikaingia *ndani* yao; bali *zikawakatia*.

58 Sasa, oneni jinsi tafsiri ya King James ingelitupa hilo: "Na ndimi zilizogawanyikana zikawajia, au kuwakalia (inasemaje katika tafsiri ya King James pale?)—zikawakalia. "Ona? Sasa, hazingeenda pale na kukaa. Twajua hilo. Lakini ile ya asili ilisema," Ukatua juu yao," naamini; sivyo? Hebu niipate sahihi hasa. Naam," . . . ukatua juu ya kila mmoja wao." Ulimi mmoja wa moto ulitua juu ya kila mmoja wao. Ona pale? Mwalifahamu? Hilo ndilo jambo la pili lililotendeka. Kwanza kulikuwa na upepo, ndipo kuonekana kwa ndimi za moto.

59 Ilikuwa katika hiki chumba kidogo hapa huku taa hizi za mafuta zikiwaka. Waza wao wakiketi pale. Na mmoja asema, "Lo!" Yeye Alitazama kote jengoni; zilikuwa jengoni kote. Kisha wakasema, "Tazama!" Ndimi za moto zikaanza ku—kuingia kote jengoni. Sasa tazama. Na kukatokea hizi ndimi za moto.

Sasa chunguza kinachofuata:

> *Kisha* . . . (Kiunganishokingine; jambo lingine likatendeka.) . . . *wote wakajazwa Roho Mtakatifu,* . . . (jambo la pili. lilichotendeka.)

60 Ona sasa, tunataka kupindua hayo tusema, "Walikuwa na ndimi za moto, huku wakitatarika; na ndipo wakatoka nje na kuanza kunena kwa lugha zisizojulikana." Hakuna kitu kama hicho Maandikoni, rafiki. Kila mmoja anayesema kwa lugha isiyojulikana anapompokea Roho Mtakatifu afanya kinyume cha Biblia. Nami nitawaonyesheni katika dakika chache na kuwathibitishieni naamini kusema katika lugha zisizojulikana,

ila huko si kupokea Roho Mtakatifu. Hiyo ni karama ya Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu ni Roho.

61 Sasa tazama. Ndimi hizi zilikuwa chumbani kama moto, na ilikalia kila mmoja. Kisha wao wakajazwa na Roho Mtakatifu (jambo la pili), ndiposa, baada ya wao kujazwa na Roho Mtakatifu, wakasema kwa lugha, si na ndimi, kwa lugha. Mlitambua hilo? Walianza kusema kwa lugha zingine kama Roho alivyowajalia kutamka. Naam, sauti hii ilisikika kote.

62 Sasa tazama. Sasa, hebu tutoe mfano tena ili msilisahau sasa. Kulingana na Maandiko, mle orofani walipokuwa wakingoja, kwa ghafula sauti kama uvumi wa upepo, uliokuwa juu yao; huo ulikuwa Roho Mtakatifu. Wangapi wanaamini huko kulikuwa kule kuonekana kwa Roho Mtakatifu? Kama upepo, upepo wa kimbinguni. Ndipo wao wakatambua. Na toka ndani ya huo mlikuwemo ndimi ndogo za moto, mia na ishirini, zikaanza kutulia na kukaa juu ya kila mmoja wao. Ilikuwa mini? Ilikuwa nini? Ile Nguzo ya Moto ambayo ilikuwa Mungu Mwenyewe akijigawanyikia Mwenyewe kati ya watu Wake, akiingia ndani ya watu. Yesu alikuwa na jambo lote; Yeye alikuwa na Roho bila kipimo; tunaipata kwa kipimo (Mwaona kile namaanisha?), maana sisi tumefanywa tu wana. Uzima Wake—Uzima Wake wa Milele ulikuwa ukiingia. Sasa, nini kilitendleka? Wao wote walijazwa na Roho Mtakatifu.

63 Sasa, nataka kuwaulizeni jambo fulani. Uvumi ulianzishwa lini? Kama iliwabidi watoke nje ya kile chumba cha orofa washukie hizo ngazi na waende kwenye jumba la mfalme—au mbele ya—ya hekalu, ambayo labda yalikuwa umbali wa jengo moja la mji toka mahali walipokuwa, orofa ya juu na ya chini, mle uwanjani ambamo watu wote walipokusanyika . . . Na wakatoka mle kama walevi waliolevywa kwa Roho. Kwa maana hao watu walisema, "Watu hawa wamelewa kwa mvinyo mpya." Hawakupata kuona jambo kama hilo.

64 Na kila mmoja alikuwa akijaribu kusema, "Roho Mtakatifu amekuja. Ahadi ya Mungu imo juu yangu. Ni—nimejazwa na Roho." Na yeye akiwa Mgalilaya, huyo ambaye alikuwa akiongea naye, Mwarabu au Mwajemi, alimsikia kwa lugha yake mwenyewe.

65 "Imekuwaje basi sisi kusikia (si lugha zisizojulikana)—imekuwaje sisi kusikia kila mtu lugha yetu tuliyozaliwa nayo? Hawa wote wasemao si Wagalilaya?" Na labda walikuwa wakinena Kigalilaya . . . Lakini walipokisikia, ilikuwa katika lugha walizozaliwa. Kama sivyo, nawatakeni mniulize—nijibuni swali hili: Ilikuwaje kwamba Petro alisimama pale na kunena katika Kigalilaya, na kundi lote liliyasikia yale aliyokuwa akisema? Nafsi elfu tatu zikamjia Kristo papo hapo na Petro akinena katika lugha moja. Hakika! Ilikuwa ni Mungu akitenda muujiza. Petro, kwa makutano wasikizi hao hao waliokuwa

wenyeji wa Mesopotamia na wageni, na waongofu, na kila mtu toka ulimwenguni kote walikuwa wamesimama pale . . . Na Petro akisimama na kuhubiri katika lugha moja na kila mtu alimsikia, kwa maana elfu tatu walitubu na kubatizwa kwa Jina la Yesu Kristo papo hapo. Na hilo je?

66 Ona, marafiki, siwezi kutarajia ndugu yangu wa kidini, Mpentekoste, kukubali hilo hivi sasa. Lakini fuatilia hayo katika Biblia nzima na uniambie wakati wo wote ambapo waliwahi kumpokea Roho Mtakatifu na kunena kwa lugha wasiyojua walikuwa wakinena nini. Na kama hiyo ndiyo njia waliyoipata pale, yale mamlaka makuu ya Mungu . . . Yabidi itendeke kila wakati vivyo hivyo.

67 Sasa, siwezi . . . Sasa, pale nyumbani mwa . . . Twakumbuka, tulipoenda kule Samaria, usiku uliopita, tuliona kwamba hakuna jambo lo lote lililoandikwa kuhusu wao kusikia kwa lugha nyingine, hakuna neno lililosemwa kuhusu hilo. Lakini walipoenda kwa nyumba ya Kornelio, ambapo kulikuwa na watu wa mataifa matatu, walinena kwa lugha. Nao walipofanya hivyo, kama walifanya hivyo, walimpokea, Petro alisema, vivyo hivyo kama wao walivyompokea mwanzoni. Nao walijua Mataifa walikuwa wamepokea neema kutoka kwa Mungu, kwa sababu walikuwa wamepokea Roho Mtakatifu kama walivyompokea hapo mwanzo. Nina swali hapa, jambo fulani juu ya hilo katika dakika chache. Nilitaka kuweka msingi, ili muone ni nini.

68 Sasa, sitarajii, watu waliofundishwa vinginevyo . . . Na nisikizeni, ndugu zangu wapendwa sana, Wapentekoste. Singefundisha hili kule nje. Hili ni . . . Singefanya lo lote kuzusha farakano. Lakini tusipopata Kweli, tutaanza lini? Yabidi jambo fulani litendeke hapa kutunyosha sisi. Yatubidi tupate neema ya kunyakuliwa hapa sasa. Yabidi Kweli ije.

69 Mtu angefanyaje kama yeye alikuwa kiziwi, na bubu, na hangenena kwa vyo vyote vile? Je yeye angempokea Roho Mtakatifu? Vipi kama yeye hana ulimi basi, na maskini hayo alitaka kuokoka? Ona? Kama Roho Mtakatifu ni ubatizo . . . Ndiposa, karama hizi zote kama kunena kwa lugha, kutafsiri lugha, ni baada ya wewe kuingia katika huo Mwili kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu. Kwa kuwa karama hizo ziko katika ule Mwili wa Kristo.

70 Sasa, sababu ya kusema . . . Sasa, tazama hapa. Ungetarajia kanisa Katoliki, ambalo lilikuwa kanisa la kwanza kuwa dhehebu ulimwenguni baada ya mitume . . . Kisha kanisa Katoliki likawa dhehebu, lo, miaka mamia kadha baada ya kifo cha mtume wa mwisho, miaka mia sita na—baada ya mitume, mara tu baada ya Baraza la Nikea, wakati wale makasisi wa Nikea walipokutana na kuunda dhehebu; ndipo—wakaweka kanisa la ulimwenguni kote, ambalo lilikuwa kanisa Katoliki. Ndani mle wakaunda kanisa la ulimwenguni. Na neno *katoliki*

maana yake ni "ulimwenguni kote;" hilo ni kila mahali wao... Warumi—Rumi ya kikafiri iligeuka ikawa Rumi ya papa. Nao wakamweka papa kuwa kiongozi kupachukua mahali pa Petro, ambapo walidhani na kusema Yesu alimpa funguo za Ufalme. Na huyo Papa alikuwa asiyeweza kukosea kamwe, na bado ingali hivyo kwa kanisa Katoliki. Kwamba...Neno lake ni sheria na taratibu. Yeye ni papa asiyekosea. Hilo likapitishwa.

71 Ndiposa, kwa maana wao hawangekubaliana na hili fundisho la Katoliki, wakauawa, wakachomwa moto, na kadhalika. Sasa sote twajua hayo kupitia kwa maandiko mastahivu ya Josephus, na *Kitabu cha Wafia Imani cha Fox* na mengine mengi yaliyo mastahivu...*Babiloni Mbili* cha Hislop, na zile—zile historia kuu. Kisha, hiyo—baada ya miaka elfu moja na mia tano, tujuavyo, ya Nyakati za Giza, watu wakanyang'anya Biblia. Na ili—ilifichwa na maskini mtawa mmoja, na kadhalika, twafahamu.

72 Ndipo baada ya hayo kukaja yale matengenezo ya kwanza ambayo yalikuwa Martin Luther. Kisha akaondoka na kusema kuwa ushirika ambao Katoliki iliuita mwili—mwili halisi wa Kristo, uliwakilisha tu mwili wa Kristo. Naye akautupa huo ushirika kwenye ubao wa madhababu, au kwenye vipandio, na kukataa kuuita mwili halisi wa Kristo, na kuhubiri, "Wenye haki wataishi kwa imani." Sasa, huwezi kutarajia kanisa Katoliki kukubaliana naye, huwezi kabisa, wakati kiongozi wao asiyekosea awaambiapo sivyo. Vema.

73 Ndipo baada ya Martin Luther, akihubiri Kuhesabiwa Haki, John Wesley akaja akihubiri Kutakaswa. Naye akahubiri kuwa mtu baada ya kutakaswa (ni vema)—lakini yakubidi utakaswe, uoshwe, shina la uovu liondolewe ndani yako kwa Damu ya Yesu. Sasa, huwezi kutarajia Mlutheri ahubiri Utakaso kwa sababu hawatafanya hivyo.

74 Baada ya Wesley kuhubiri Utakaso, na vikundi vingi vilivyojitenga nacho, ambamo mlitokea Methodisti ya Ki—Wesley, na Wanazarini, na kadhalika, waliouendeleza moto katika wakati wao, kisha ikaja Pentekoste na kusema, "Naam, Roho Mtakatifu ni ubatizo, na tunanena kwa lugha tunapompokea." Hakika. Ndipo hilo lilipojitokeza, hungetarajia Wanazarini, na Wamethodisti ya Wesley, na wengineo kuamini hilo. Wao hawangelifanya hivyo. Waliliita ibilisi. Vema. Nini kilitendeka? Wakaanza kuanguka; Wapentokoste wakaanza kuinuka. Sasa imefikia mahali ambapo hata Pentekoste imetikisika. Imeunda dhehebu na kutoka nje, hawakubali kingine cho chote. Wana sheria na kanuni zao wenyewe, na hilo latosheleza.

75 Sasa, Roho Mtakatifu aingiapo na kufunua Kweli ya jambo lo lote na kulithibitisha kwa Uwepo Wake Mwenyewe na kwa Neno Lake, huwezi kutarajia Wapentekoste waseme,

"Nitakubaliana nalo." Yakubidi usimame peke yako kama Luther alivyofanya, kama Wesley alivyofanya, na kama wengine wao wote walivyofanya. Yakubidi kusimama kwa hilo kwa sababu wakati huo umefika. Na hilo ndilo hunifanya nionekane mjinga. Hilo ndilo linalonifanya kuwa tofauti.

76 Nami siwezi kuanza kama Ndugu yangu mpendwa Oral Roberts, na Tommy Osborne, Tommy Hicks, na wengineo, kwa sababu makanisa hayatakubaliana nami. Wao wanasema, "Yeye huamini usalama wa milele. Yeye ni Mbatisti. Yeye haamini kunena kwa lugha kama ishara madhubuti ya Roho Mtakatifu. Mwacheni mtu huyo! Ona?

77 Lakini kabiliana uso kwa uso nayo. Ikabilie vilivyo. Wanaweza kukabiliana na Walutheri, Wa—Wamethodisti wanaweza. Wapentekoste wanaweza kukabiliana na Wamethodisti. Naweza kukabiliana na Wapentekoste nayo. Ni kweli hasa. Ni kweli. Mbona hivyo? Tunatembea katika Nuru kama Yeye alivyo katika Nuru. Ona? Tunatembea kwenye Barabara kuu ya Mfalme, na inavyozidi kusonga mbele ndivyo neema zaidi inavyotolewa, nguvu zaidi zinatolewa, ya kimbunguni zaidi yanatolewa. Na tuko pale. Hii ni saa ambayo Roho Mtakatifu amekufa kwa mfano wa Nuru kama alivyokuwa mwanzoni, Nguzo ya Moto, na amejidhihirisha Mwenyewe, akifanya mambo yale ambayo Yeye alifanya alipokuwa hapa duniani. Na Yesu alisema, "Unajuaje kama ni wa kweli au la? Kwa matunda yao mtawajua. Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio."

78 Sasa, ndugu zangu Wapentekoste. Mimi niko pamoja nanyi. Mimi ni mmoja wenu. Nina Roho Mtakatifu. Nimenena kwa lugha, ila sikuipata nilipompokea Roho Mtakatifu. Nilipokea ubatizo wa Roho Mtakatifu; nikanena kwa lugha, nikatoa unabii, nilikuwa na karama za maarifa, hekima, tafsiri, na kila kitu kikitendeka. Lakini nina haki kwa kila moja ya vitu hivyo, kwa sababu mimi sasa ni mwana wa Mungu. Ile nguvu, ule Moto wa Mungu uko nafsini mwangu; huo ulimi wa Moto uliowaka—uliingia ndani yangu na kuteketeza kila kitu kilichokuwa kinyume cha Mungu, na sasa naongozwa na Roho Wake. Yeye angesema, "Kwenda *hapa*," nami nitaenda. "Kwenda *hapa*;" nami nitaenda. "Nena *hapa;"* nitanena. "Na fanya *hiki, kile* na *kinginecho."* Naam, kama tu. . . Unaongozwa na Roho. Huyo ni Mungu ndani yako, akitenda mapenzi Yake, haijalishi ni nini, Yeye anafanya mapenzi Yake.

79 Sasa sikiza. Hebu nione—nisome hapa katika kamusi hii hapa kabla sijaanza swali lile. Sasa toka kwa Tafsiri ya Vatikani chuo cha 7, 190-1205:

> "Ni vigumu kuamua kama ilikuwa sauti za *hao watu* zikinena katika *lugha ya kigeni;* au habari au uvumi

wa matendo ya ule *upepo* wa kimbinguni ukivuma *uliowasisimua makutano hayo*."

Hawangelifahamu. Sasa tazama. Au ilikuwa ni watu . . .

80 Nitaeleza tu kwa mfano. Hapa kuna kundi la maskini Wagalilaya ovyo. Na hapa wao walikuwa nje pale katika njia za mji. Hawakuwa wamewahi kuona kitu kama hicho; mikono yao ikiwa juu hewani, walikuja toka kwa kile chumba cha orofa, wakashuka kwa ngazi, nje mle, wamejazwa tu: walikuwa bado hawajanena. Ona? Ndio hao wanashuka mle. Na sasa, hebu tuseme, walikuwa nje pale wakipepesuka hapa na pale kwake. Na hao watu wakasema . . . Myunani alinijia mbio na kusema, "Nanena Kigalilaya."

Ukakimbia mbio alipo na kusema, "Namna gani wewe, Kijana?"

81 "Nimejazwa na Roho Mtakatifu. Nguvu za Mungu zilishuka mle chumbani. Kitu fulani kilitendeka kwangu. Ee, Mungu atukuzwe!"

Na mwingine juu hapa, yeye alikuwa akiongea na Mwarabu, naye ni Mgalilaya akiongea Arabu—lugha ya Kiarabu.

82 Sasa, hawawezi kupambanua, je, ni upepo unaovuma uliowaleta watu pamoja wakati umati ulipokusanyika, au ilikuwa ni kunena kwa lugha ng'eni waliyokuwa wakinena? Sasa, Biblia haisemi hasa . . . Kuna vitu wiwili uwezavyo kutazama. Ilikuwa ni . . . Wale—wale wa nje walisema, "Imekuwaje basi sisi kusikia kila mtu kwa lugha yetu tuliyozaliwa nayo?" Haikusema walikuwa wakiinena, lakini walikuwa wakiisikia.

83 Kisha kundi lile lile, watu wale wale walieleza hili. Petro aliruka juu ya kitu fulani na kusema, "Enyi watu wa Galilaya, na ninyi nyote mkaao Yerusalemu, lijueni jambo hili, (watu husema hawakuwa na lugha ya Kigalilaya) lijueni hili, mkasikize maneno yangu (alikuwa akinena lugha gani, kwa hao wote?); Naam, sivyo mnavyodhani, watu hawa hawakulewa, kwa maana ni saa tatu ya mchana; lakini jambo hili ni lile lililonenwa kwa kinywa cha nabii Yoeli: "Itakuwa siku za mwisho, asema Mungu, nitawamwagia watu wote Roho Yangu, na wana wenu na binti zenu watatabiri." Akaendelea na kuendelea, na kusema, "Ninyi mmemsulubisha kwa mikono ya watu wabaya yule Mwana wa Mungu asiye na hatia. Daudi alitaja habari zake . . . 'hutaiacha roho Yake katika kuzimu, wala hutamtoa Mtakatifu Wako aone uharibifu." Na kasema, "Na mjue yakini ya kwamba Mungu amefanya Yesu huyo mliyemsulubisha kuwa Bwana na Kristo." Na waliposikia haya . . . Amina! Nani? Kila mtu chini ya mbingu. Nini ilikuwa ikitendeka? Yeye hakuwa akisema, "Sasa, nitaongea Kigalilaya; nitanena *hii;* nami nitanena kwa *hii . . . ? . . .*

84 Petro alipokuwa akinena maneno haya, wao walisema, “Enyi waume na ndugu tutendeje tupate kuokoka?” Na Petro aliwapa huo utaratibu. Hivyo ndivyo inavyotendeka kila mara. Ona?

85 Inaelekea juu, kujitahidi iingie ndani ya Mungu, kutembea karibu. Unajuaje? Vema sasa, Luther alipopokea Kuhesabiwa Haki, yeye aliita huko Roho Mtakatifu. Ilikuwa hivyo. Mungu alichovya kidogo ndani Yake. Kisha yeye alisema nini? Wesley alipokea Utakaso, na kusema, “Wee, unapopaza sauti, umempokea.” Lakini wengi wao walipaza sauti ambao hawakuwa naye. Wapentekoste waliponena kwa lugha—lugha zisizojulikana, wao walisema, “Wee, umempokea.” Lakini wengi wao hawakumpokea.

Hakuna kitu kama ishara hizo za kujua hilo. Njia pekee ujuayo mti,” Yesu alisema, “ni kwa matunda uzaayo,” kazi za Roho, matunda ya Roho. Basi umwonapo mtu aliyejazwa na nguvu, aliyejazwa na Roho Mtakatifu, ndipo unaona maisha yaliyobadilika. Unaona ishara hizi zikifuatana na hao waaminio: “Kwa Jina Langu watatoa pepo, watasema kwa lugha mpya. Nyoka akiwauma, hatawadhuru. Kama wamekunywa kitu cha kufisha, wakinywa, hakitawadhuru. Wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya.” Lo! Ishara za namna hii hufuatana na hao waaminio. Lakini unaingiaje ndani yazo? Karama hizo ziko katika Mwili ule. Unaingiaje katika Mwili ule? Si kwa kunena hata ukaingia; bali kwa kubatizwa katika Mwili mmoja (I Wakorinto 12:13). Roho mmoja sisi sote tumebatizwa katika Mwili huo na tukaruhusiwa karama zote. Bwana awabariki.

86 Sasa, mtu akisikiza ukanda huu au mtu ye yote hapa asipokubaliana nami; kumbuka, fanya hivyo kwa upendo, ndugu, kwa sababu nawapenda.

93. Swali la kwanza usiku huu: **Ndugu Branham, nadhani televisheni ni laana kwa ulimwengu. Unaonaje hilo?**

87 Vema, ye yote yule aliyeandika hili, nitakubaliana nawe, wameifanya laana kwa ulimwengu. Ingekuwa baraka kwa ulimwengu, lakini wameifanya laana. Kitu kama hicho, watu wangu wapendwa, ni kile wewe mwenyewe unachotazama. Kama televisheni ni laana, basi magazeti ni laana, basi redio ni laana, na wakati mwingi simu vile vile. Ona, ona, ona, ona? Ni kile unachotaka humo. Lakini kwa kuwa ndugu alisema usiku uliopita, kuwa ni vigumu kupata vipindi tena kwenye televisheni; hicho kinagharimu pesa nyingi sana. Mhubiri maskini ahubiriye Injili Nzima hawezi kulipia kipindi kwenye televisheni. Kwa hivyo basi. . .Ndugu alisema usiku uliopita, naamini, au mahali fulani. “Panguzeni redio zenu,” au mtu fulani, au, “Itoeni mle pembeni na msikize vipindi hivyo.” Naam.

88 Lakini, mtu mpendwa, ye yote uliye, nakubaliana nawe bila shaka. Imekuwa mojawapo wa vitu vilivyolaaniwa sana

kwa binadamu. Ndani mle wanachukua pesa hizi zote ambazo zingeenda serikalini kwa kodi, na kuzitumia kwa matangazo ya biashara ya hivi vipindi vya sigara na mvinyo na mengineyo kama hayo, na kuepa kodi za serikali; ndiposa wanakuja na kuwapata wahubiri na kuwaingiza mahakamani wapate kwao pesa ndogo. Nakubaliana nawe, ni jambo mbaya sana. Sasa, hilo si . . . Mwajua, ni kitu fulani tu upatacho. Asante, Dada, Ndugu, yeye yote yule aliyeuliza swali hilo.

94. Sasa, hapa kuna nzuri. Swali: **Kuna mahali katika Biblia kama I Samweli 18:10, ambapo panasema pepo mchafu kutoka kwa Mungu alifanya mambo. Sifahamu "pepo mchafu kutoka kwa Mungu." Tafadhali fafanua hili.**

89 Vema, labda kwa msaada wa Bwana, naweza. Haimaanishi kuwa Mungu ni pepo mchafu. Lakini kila pepo wa kila kitu yumo chini ya mamlaka ya Mungu. Na Yeye hufanya kila kitu kifanyike kulingana na mapenzi Yake. Ona?

90 Sasa, kuhusu swali lako, unanena kuhusu roho mchafu aliyetoka kwa Mungu kumtesa Sauli. Yeye alikuwa na moyo mzito amevunjika moyo na—kudhoofika, kwa sababu kwanza, alikuwa ameanguka. Na unapoanguka, roho mchafu—Mungu ataruhusu roho mchafu akutese.

91 Ningependa kuwasomeeni kitu fulani katika—katika dakika chache. Nina wazo lingine juu ya hili hapa. Ona? Kila roho yabidi awe chini ya mamlaka ya Mungu. Mwakumbuka wakati Yehoshafati na Ahabu walikuwa wakienda vitani? Na muda si muda, kulikuwa na—wao walikuwa wameketi kwenye malango. Na Yehoshafati alikuwa mtu mwenye haki, naye akasema (wale wafalme wawili waliketi pale, nao wakaunganisha majeshi yao pamoja)—basi akasema, "Hebu tu mulize Bwana kama tutaenda ama hatuendi."

92 Na Ahabu akaondoka akawachukua manabii mia nne aliokuwa nao, wote aliowalisha na kuwanonesha na kila kitu; wao walikuwa wenye afya nzuri. Nao wakaja pale, nao wote wakatabiri kwa nia moja, wakisema, "Kwea, na Mungu atakupa ushindi. Kwea Ramothi-Gileadi na kule Mungu atakutwalia kitu kile." Mmoja wao alijitengenezea pembe mbili na kuanza kukimbia hapa na pale kama mfano wake, kasema, "Kwa hizi pembe za chuma, utawasukuma kabisa toka nchi ile; ni yako."

93 Lakini mwajua, kuna kitu fulani kuhusu mtu wa Mungu ambacho hakikubaliani na hayo yote. Ona? Kama hayalingani na Maandiko, mna kasoro fulani. Mwamini ye yote wa kweli . . . Kwa hivyo Yohoshafati akasema, "Vema, hao mia nne wanaonekana sawa. Wanaonekana watu wazuri."

"Ee, ndiyo," labda Ahabu alisema hivyo.

Lakini Yohoshafati akasema, "Je, huna mmoja zaidi?" Mbona mmoja zaidi hali una mia nne walio na nia moja?

Kwa maana yeye alijua kulikuwa na kitu fulani ambacho hakikuonekana sahihi. Ona?

Yeye alisema, "Naam, tuna mmoja zaidi, mwana wa Imla, juu hapa," Kasema, "Lakini namchukia." Hakika. Atalifunga kanisa lake wakati wo wote awezao. Atamfukuza nchini. Ona? "Hakika, namchukia."

"Mbona unamchukia?"

"Yeye kila mara hunibashiria mabaya." Naamini Yehoshafati alijua papo hapo kulikuwa—kitu fulani hakikuwa sahihi.

Kwa hivyo yeye alisema, "Kwea kamlete Mikaya."

Kwa hivyo wakaondoka kwenda kumleta, naye ndiye huyu akija. . . Kwa hivyo walipokwenda kule wakamtuma mjumbe wakisema, "Basi, hebu kidogo. Naam, wao wana Madaktari wa Theologia mia nne kule. Hao ndio bora sana walioka nchini, wenye PH, LLD, na kadhalika." Kasema, "Sasa, wajua, wewe ambaye ni mtu maskini asiyeelimika, hutakataa kukubaliana na hao makasisi.'

94 Imla alisema hili, au namaanisha, Mikaya alisema hili: "Sitasema lo lote hata Mungu atakapoliweka kinywani mwangu, na ndipo nitasema yale hasa asemayo." Napenda hilo. Napenda hilo. Yaani, "Nitakaa na Neno." Haijalishi wengine wao wanasema nini, yeye alisema, "Vema," kasema, "nakwambia. Kama unataka kutupwa nje, heri useme lile lile."

Kwa hivyo yeye akashuka kwenda pale. Basi akasema, "Je! nikwae?"

Yeye akasema, "Endelea." Kasema, "Mnipe usiku huu. Hebu na niongee na Bwana." Napenda hilo. Kwa hivyo usiku huo Bwana akamtokea, na siku iliyofuata akaamka. Naye alisema, alipokuwa akikwea, kasema, "Endelea; bali naliwaona Israeli kama kondoo wasio na mchungaji, wametawanyika mlimani." Jamani! Hilo lilimkatiza pumzi.

Naye alisema, "Je! sikukwambia? Nalijua. Hivyo ndivyo yeye afanyavyo wakati wote, kusema jambo baya kunihusu mimi."

95 Mbona? Yeye alikuwa akiduma kwa Neno. Mbona? Nabii aliyemtangulia, Neno la Mungu likija toka kwa Eliya, nabii halisi, alisema, "Kwa sababu umemwaga damu ya Nabothi asiye hatia, mbwa watalamba damu yako pia." Naye alimwambia mabaya. Elisha alikuwa amekwisha kwenda Mbinguni. Lakini twajua kuwa Elisha alikuwa na Neno la Mungu, kwa hivyo yeye alidumu kwa Neno. Napenda hilo. Kaa na hilo Neno.

96 Kama Biblia ilisema Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo na hata milele; Nguvu Zake zingali zile zile; Roho Mtakatifu ni kwa ye yote atakaye, na aje, dumuni katika Neno. Naam, bwana! Haijalishi wengine wao wasema nini. Vipi wamelishwa vema na wamepitia shule ngapi, hilo halihusiani nalo.

Kwa hivyo yeye alisema. . .mtu huyu mkuu mwenye pembe kichwani mwake, akienda kusukumia—nchi ile toka kwa mfalme, yeye alienda pale na kumpiga kofi mdomoni (huyu mhubiri mdogo). Yeye alijua alikuwa tu mtakatifu anayejigaragaza kwa hivyo hakungesemwa lo lote, kwa hivyo akampiga kofi mdomoni. Yeye akasema, "Nataka kukuuliza kitu fulani." Kasema, "Roho wa Mungu alienda njia ipi aliponiondoka mimi kama unaye?"

97 Yeye alisema, "Utafahamu utakapokuwa umeketi tunduni kule kama mateka." Yeye alisema, "Nilimwona Mungu ameketi katika kiti cha enzi (Amina! sasa sikiza!), na majeshi ya Mbinguni wamemzunguka." Ilikuwaje? Nabii Wake alikuwa amekwisha sema yale yangetendeka kwa Ahabu. Mungu. . . Huyo hakuwa Eliya aliyeyasema hayo; huyo alikuwa yule nabii aliyepakwa mafuta. Hilo lilikuwa Neno la Bwana, BWANA ASEMA HIVI. Na Mikaya alisema, "Niliona majeshi yote ya Mbinguni yamekusanyika kumzunguka Mungu katika mkutano mkubwa. Nao walikuwa wakisemezana wao kwa wao. Na Bwana akasema, 'Nani anayeweza kushuka kwenda—nani kati yenu anayeweza kushuka aende akamdanganye Ahabu, kumpeleka kule nje kutimiliza Neno la Mungu, akauawe? Nani tutakayemtuma kule!"

98 Basi, huyu alikuwa anasema *hilo* au *lile*. Na baada ya muda mchache, pepo mchafu, pepo wa uongo akajitokeza kutoka chini na kusema, "Ukiniruhusu tu. Mimi ni pepo wa uongo. Nitashuka na kuwaingia wahubiri hao wote, kwa sababu hawana Roho Mtakatifu; na nitawafanya (wao ni vijana tu waliofundishwa shuleni)—nami nitashuka, na kuingia katika kila mmoja wao, na kuwadanganya, na kuwafanya wabashiri uongo." Je, yeye alisema hilo? Basi akasema, "Hivyo ndivyo tutakavyodanganya." Kwa hivyo yeye akashuka kwenda kule.

Yeye alisema—Mungu alisema, "Una ruhusa Yangu kuenda."

99 Naye alishuka akaenda na kuwaingia hao manabii wa uongo, huduma iliyofundishwa shuleni, na kuwafanya wabashiri uongo. Ilikuwa ni pepo wa uongo akifanya mapenzi ya Mungu Hebu ni. . .kitu fulani tu ambacho huenda uka-. . .Ona hapa, kwa dakika moja hivi. Tazama hili. Nawatakeni mfunue pamoja nami katika I Wakorintho sura ya 5, kifungu cha 1, kwa dakika moja tu. I Wakorintho. . .Basi tazama hili ukitaka kuona kitu fulani, Mungu akifanya jambo—jinsi hao pepo wachafu, jinsi wata—watatenda. . .vema, Paulo akinena:

> *Lakini habari imeenea ya kuwa kwenu kuna zinaa, na zinaa ya namna isiyokuwako hata. . .katika Mataifa,* (wawazaje kuhusu hilo katika kanisa?). . .*kwamba mtu awe na mke wa babaye.*
>
> *Nanyi mwajivuna, wala ham—*. . .(Hebu tuone. Naamini nilifungua kurasa mbili kwa. . .). . .*Nanyi—*

> *nanyi mwajivuna, wala hamkusikitika, ili kwamba*. . . (Sasa, ngoja kidogo hapa. Nina. . .Naam, ndivyo. Naam.). *hamkusikitika*. . .(Ndivyo.). . .*mwajivuna, wala hamkusikitika, ili kwamba aondolewe miongoni mwenu huyo aliyetenda jambo hilo.*

100 Ni—sijui. Siamini kuwa mtu ye yote angenena haya wala kuyakatiza, lakini nashuhudia tu yale ninayoamini: Mtu akijazwa mara moja na Roho yeye hawezi kumpoteza. Ona, Ona?

> *Kwa maana kweli, nisipokuwapo kwa mwili lakini nikiwapo kwa roho, mimi mwenyewe nimekwisha kumhukum yeye aliyetenda jambo hilo, kana kwamba nikiwapo.*
>
> *Katika jina la Bwana wetu Yesu Kristo, ninyi mkiwa mmekusanyika pamoja, na roho yangu, pamoja na uweza wa Bwana wetu Yesu Kristo;*
>
> *Kumtolea shetani mtu huyo, ili mwili uadhibiwe, na roho iokolewe katika siku ya Bwana Yesu.*

101 Mungu, akiliambia Kanisa takatifu, ambalo ni Mwili Wake hapa duniani, kuwa (sasa, hili ni baada ya Agano la Kale, katika lile Jipya)—akimwambia mtu aliyekuwa mchafu sana na mwovu kati ya watu hata akazini na mke wa baba yake mwenyewe. Kasema, "Kitu kama hicho katika Mwili wa Kristo. Ninyi, Kanisa, mtoleeni shetani kwa ajili ya kuadhibiwa. . ." Ona? Mungu hukubalia. . .Naye akiwa na jambo fulani analotaka litendwe, kumchapa mjeledi mtu fulani, Yeye atamwachilia pepo mchafu kwake ili wamtese mtu huyo na—na kuwarudisha. Sasa, twaona ya kwamba mtu huyu baada. . .

102 Hiyo ndiyo shida ya makanisa siku hizi, mtu ajapo katika Mwili wa Kristo na kuwa mmoja wa washiriki na kuanza kufanya mabaya, badala ya ninyi nyote kukutanika pamoja na kutenda jambao lili hili. . .Na ninyi, Maskani ya Branham, fanyeni hilo. Kwa sababu mradi tu mnamshikila, yeye yuko chini ya ile Damu. Na yeye anaendelea kufanya jambo lile la kale tena na tena na tena wakati wote. Kutanikeni pamoja na kumtolea kwa shetani ili mwili uharibiwe, ili roho yake ina—ipate—iokolewa katika siku ya Bwana. Na tazama mjeledi wa Mungu ukija. Mtazame shetani akimshika. Hiyo ni pepo mchafu anayempata.

103 Na kijana huyu hapa akanyosheka. Akarudi. Twaona katika 2 wakorintho ambapo yeye ametakasika vilivyo mbele za Mungu.

104 Mtazame Ayubu, mtu mkamilifu, mtu mwenye haki. Na Mungu aliruhusu shetani mwovu amjie, na kumrudi, na mengineyo kwa ajili ya kukamilishwa kwa roho yake. Ona? Kwa hivyo pepo mchafu ana. . .Mungu hutumia pepo wachafu mara nying kutekeleza mpango Wake na mapenzi Yake.

95. Sasa, hapa kuna moja gumu sana. Swali (Nadhani ni mtu yule yule, kwa sababu inaonekana kama mwandiko ule ule): **Kama yambidi mtu kuwa na Roho Mtakatifu ku—kuwa na Roho Mtakatifu ili aongoke na apate kunyakuliwa, itakuwaje kwa watoto ambao wamekufa kabla miaka ya kujua mema na mabaya? Nao watafufuka lini?**

105 Sasa, ndugu, dada, siwezi kukwambia hilo. Hamna Andiko po pote katika Biblia niwezalo kupata. Lakini naweza kueleza mawazo yangu. Sasa, hili litakuimarisha wewe unayeamini katika neema ya Mungu. Mwaona, mtu huyo ataka kujua (ambalo ni swali nzuri sana. Ona?)—mtu huyu ataka kujua ufufuo gani—itakuwaje kwa mtoto mchanga, kama kwamba yambidi yeye awe na Roho Mtakatifu kusudi apate kunyakuliwa . . . Kama nilivyosema, naam. Hilo ni kulingana na Biblia. Hilo ni fundisho la Maandiko. Si ku—si kuenda Mbinguni . . . Kwa sababu watu waliojazwa na Roho Mtakatifu ni ule ufufuo wa kwanza, walio Wateule. Na waliosalia wa wale . . . Hao wafu waliosalia hawakuwa hai, hata itimie ile miaka elfu. Baada ya ule Utawala wa Miaka Elfu, ndipo ule ufufuo wa pili, ile hukumu ya kile Kiti Cheupe cha Enzi, ona? Hiyo ndiyo taratibu ya Biblia hasa. Lakini mtu huyu ataka kujua itakuwaje kwa hawa watoto wachanga. Wao . . . Yaani, je, walikuwa na Roho Mtakatifu kabla hawajazaliwa? Je, walimpokea? Sasa, hilo siwezi kuwaambieni.

106 Lakini sasa, hebu tuseme hivi: Twajua kuwa watoto wachanga wanapokufa, bila kufikiri ya wazazi wao, wao wameokoka. Sasa, sikubaliani na mafundisho ya manabii juu ya hilo. Wanasema kama ingekuwa—walikufa wakiwa na wazazi ambao ni wenye dhambi, kwamba mtoto huyo angeenda kuzimuni, angeoza; angeangamia kabisa. Vema, Yesu . . . Yohana alisema Yesu alipokuja, "Tazama Mwana-kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi za ulimwengu." Na kama mtoto huyo alikuwa mwanadamu, ambaye ingebidi aje chini ya hukumu za Mungu, na Yesu alikufa kuondoa dhambi, dhambi zote ziliondolewa, mbali mbele za Mungu wakati Yesu alipokufa kwa kusudi hilo. Dhambi zako zilisamehewa. Dhambi zangu zilisamehewa. Na jinsi tu unavyoweza kusamehewa ni kukubali msamaha Wake. Sasa, mtoto hawezi kukubali masamaha Wake, kwa hivyo hajafanya lo lote. Hajafanya lo lote kamwe. Kwa hivyo yu huru kabisa kwenda Mbinguni.

107 Lakini utasema, "Je, watanyakuliwa?" Sasa—sasa hili ni neno langu mwenyewe: hili ni wazo langu sasa. Usi . . . Siwezi kuthibitisha hili kwa Biblia. Lakini tazama. Kama Mungu, kabla dunia kuwekwa misingi, alimjua kila mwanadamu atakayewahi kuwepo duniani. Je, mwaamini hilo? Yeye alijua kila mbu, kila kiroboto, kila inzi, Yeye alijua kila kitu amabacho kingekuwako duniani. Kama Yeye alijua hilo.

108 Tazama. Hebu tuchukue kwa mfano, Musa. Musa alipozaliwa, yeye alikuwa nabii. Kabla Yeremia... Mungu alimwambia Yeremia, "Kabla hata hujakuwepo tumboni mwa mama yako, kabla hujakuwepo tumboni mwake, nalikujua, na kukutakasa, na kukuweka kuwa nabii wa mataifa." Yohana Mbatizaji, miaka 712 kabla hajazaliwa, Isaya alimwona katika ono, kasema, "Yeye ni sauti ya mtu aliaye nyikani."

109 Kule kuchaguliwa tangu asili au kujua tangu asili kwa Mungu kwajua yote kuhusu watoto wachanga (ona?), yale wao ilikusudiwa wafanye. Naye alijua wangekufa. Yeye alijua. Hakuna kitu kiwezacho kutendeka pasipo Mungu kujua habari zake. Hakuna kitu kiwezacho kutendeka kwa... Kama tu Mchungaji Mwema jinsi anavyoingia... Naam, kuchukua hili kwa Andiko singalisema Maandiko yasema *hivi na vile*. Nalitoa tu mawazoni mwangu.

96. Sasa, swali linalofuata ni lile ambalo nadhani labda mtu fulani alikuwa—yale niliyonena usiku mwingine. **Eleza mke kuokolewa kwa kuzaa mtoto.**

110 Mwanamke haokolewi kwa kumzaa mtoto. Lakini hebu tufungue sasa I Timotheo 2:8 kwa dakika moja hivi. Na hebu tuone yale Biblia inasema kuhusu mtoto. Sasa, natambua hilo ni fundisho la Katoliki, kwamba Wakatoliki husema mwanamke anaokolewa kwa uzazi, kwa kuzaa mtoto. Lakini hebu tusi... Siamini hilo. I Timotheo sura ya 2, na hebu tuanzie kifungu cha 8, na tusome kidogo sasa. Vema, sikiza.

> *Vivyo hivyo wanawake na wajipambe kwa mavazi ya kujisitiri*... (Haitupasi kuswali hilo, sivyo? Sikiza hili.)... *pamoja na adabu nzuri,*... (Whiu!)... *na moyo wa kiasi, si kwa kusuka nywele, wala kwa dhahabu na lulu, wala kwa nguo za thamani;* (Ndugu, nawasaidieni ninyi hapa, natumai. Hizi kofia mpya kila siku au siku tatu. Mwaona? Hayo hayampasi Mkristo.)
>
> *Bali (kwa matendo mema, kama iwapasavyo wanawake wanaoukiri uchaji wa Mungu)* na matendo mema.
>
> *Mwanamke na ajifunze katika utulivu, akitii kwa kila namna.*
>
> *Simpi mwanamke ruhusa ya kufundisha, wala kumtawala... mwanamume, bali awe... katika utuiivu.*
>
> *Kwa maana Adamu ndiye aliyeumbwa kwanza, na Hawa baadaye.*
>
> *...Adamu hakudanganywa, ila mwanamke alidanganywa kabisa akaingia katika hali ya kukosa.*
>
> *Walakini ataokolewa kwa uzazi wake kama*... (Sasa, yeye haongei kuhusu mwanamke wa kilimwengu

kupata watoto.)...*Kama akidumu katika imani*... (Ona? kama akidumu. Yeye amekwisha kuwemo... Huyo ndiye mwanamke anayenena habari zake, mwanamke ambaye amekwisha okoka. Ona?)...*na upendo na utakaso, pamoja na moyo wa kiasi.*

111 Si kupata mtoto kunakomfanya mwanamke aokoke, bali ni kwa sababu yeye anawalea watoto, akitimiza wajibu wake, si kulea paka, mbwa, na kadhalika kupachukua mahali pa mtoto, kama wafanyavyo siku hizi, kumpea upendo wa mama ili yeye apate kwenda na kuzurura usiku kucha. Watu wengine hufanya hivyo. Niradhini, bali wao hufanya hilo. Huo ni utovu wa adabu kwangu kusema, lakini kweli ni kweli. Ona? Hawataki mtoto wa kumfunga wakati wote. Lakini kwa uzazi, kama akidumu katika imani, utakaso, na moyo wa kiasi, ataokolewa. Lakini ile kama ni, utaokolewa pia, kama umezaliwa mara ya pili. Uta—unaweza kuponywa kama ukiamini. Unaweza kumpokea Roho Mtakatifu ukimwamini, umjitayarishie kama uko tayari kumpokea. Basi ataokolewa kama akiendelea kufanya mambo haya (Ona?), lakini si kwa kuwa eti yeye ni mwanamke. Kwa hivyo hilo ni sawa, ndugu, dada. Si mafundisho ya Katoliki kwa vyo vyote vile. Sasa, nataka...Hapa kuna jingine lenye kunata. Kisha tuna moja zaidi. Nafikiri labda tuna wakati kwa ajili yake. Nilichukua tu wakati wetu. Sasa, hili ni—hili ni matokeo ya mkutano wa ufufuo. Haya ni matokeo ya mkutano ule, maswali haya.

97. Sasa, Ndugu Branham (limepigwa chapa)**, ni la Kimaandiko kwa mtu kunena kwa lugha na kutafsiri ujumbe wake mwenyewe? Kama ndivyo, tafadhali eleza 1 Wakorintho— au Wakorintho 14:19 na pia Wakorintho 14:27.**

112 Vema hebu tuendee Andiko hilo na kuona yale lisemayo. Ndiposa tutaona kama tunalitii hili Kimaandiko. Tunataka kila mara kuwa wa Kimaandiko. Basi Wakorintho 14. Sasa mtu yule ataka kujua kama ni la Kimaandiko kwa mtu kutafsiri ujumbe wake mwenyewe aliounena kwa lugha. "Kama hivyo, eleza Wakorintho 14:19," Hebu tuone, 14 na 19. Vema, tumepapata.

Lakini katika kanisa...napenda kunena maneno matano kwa akili zangu, nipate kuwafundisha wengine, zaidi ya kunena maneno kumi elfu...kwa...kwa lugha.

Sasa, kinachofuata ni kifungu cha 27, wanataka kujua.

Kama mtu akinena kwa lugha, wanene—wawili au wa watatu, si zaidi, tena zamu kwa zamu na mmoja na afasiri.

113 Sasa, nachukua yale mtu yule anayojaribu kufikia (ambayo nataka—nanaenda kuwasomeeni ninyi kitu fulani hivi punde). Lakini nadhani yale ndugu au dada anajaribu kufikia, "Ni sahihi kwa mtu anayenena kwa lugha pia kutafsiri ujumbe ambao

yeye ameunena?" Sasa, rafiki mpendwa sana, kama utasoma kile kifungu cha 13 katika sura ile ile, kitakwambia:

> *Kwa sababu hiyo yeye anenaye kwa lugha na aombe apewe kufasiri.*

114 Hakika, yeye anaweza kutafsiri ujumbe wake mwenyewe. Sasa, kama tuki . . . Hebu tu . . . Vema, wewe . . . Soma yote hapa, nawe unaweza kuona ni . . . Hebu soma sura hiyo yote. Ni nzuri sana, na inalieleza.

115 Sasa, kunena kwa lugha . . . Sasa, hali tukiwa kwa hilo, na hili likiwa linanaswa kwenye kanda, nataka kusema naamini kunena kwa lugha zaidi tu kama ninavyoamini uponyaji wa Kiungu, na u—ubatizo wa Roho Mtakatifu, kuja kwa pili kwa Kristo, na nguvu za zamani zijazo; naamini hayo zaidi tu kama ninavyoamini, lakini naamini kunena kwa lugha kuna mahali pake kama tu kule kuja kwa Kristo kulivyo na mahali pake; uponyaji wa Kiungu una mahali pake; kila kitu kina mahali pake.

116 Sasa, kwenu watu, nina nafasi ya kusema hili sasa, nami ningetaka kulieleza. Na kama nimemuudhi mtu ye yote, sikusudii hivyo. Sikusudii hivyo. Sikusudii kuzusha mafarakano. Lakini sikiza. Imekuwaje kunena kwa lugha zisizojulikana kwa Wapentekoste—(ambao ni mimi mwenyewe; Mimi ni Mpentekoste. Ona?) . . . Basi, shida yake imekuwa hii: kuwa—hawakuheshimu. Na jambo lingine, wanaacha tu zinenwe bila taratibu. Hawarejei kwa Neno.

117 Sikiza sasa. Hapa kuna njia—hebu—hivi ndivyo kanisa linavyoimarishwa. Sasa, katika kanisa la Kipentekoste, kama ningalikuwa mchungaji wa kanisa hili, ningewaambieni jinsi mngeliliimarisha (Ona?), kama ningekuwa—ningalikuwa hapa wakati wote kulichunga. Ningekubali kila karama katika Biblia. Niwaambie waamini kwanza wabatizwe kwa Roho Mtakatifu. Ndiposa, bila shaka kila karama ya 1 Wakorintho 12 ingekuwa ikifanya kazi katika kanisa langu, kama ningewaingiza mle, mwili wote ukitenda kazi.

118 Sasa, ukichunguza . . . Si kutoa matamshi sasa. Na kumbuka, singesema neno moja kinyume chake—labda ningemkufuru Roho Mtakatifu. Na Mungu ajua singesema hilo vibaya. Ona? Lakini ninasema tu hili kwa kujaribu kuwapeni ninyi mtazamo wa Maandiko baada ya mimi kuyasoma kirefu sasa kwa karibu miaka ishirini. Nimekuwa nikihubiri kwa karibu miaka thelathini. Nami nimepitia katika kila jambo, nikafaulu kwa shida; unaweza kuwaza jinsi imekuwa. Nikimchunguza kila mtu, na mafundisho, ulimwenguni kote. Nikifanya hivyo kwa sababu hunivutia. Ni muhimu kwa wanadamu mbali nami mwenyewe. Yanibidi niondoke hapa. Yakubidi uondoke hapa. Nami nikiondoka kama nabii wa uongo, nitaipoteza nafsi yangu mwenyewe na kupoteza zenu pamoja na yangu. Kwa hivyo ni

zaidi ya—ni muhimu kuliko chakula cha kila siku; ni zaidi ya sifa; ni zaidi ya kinginecho cho chote; ni uzima kwangu. Ona? Nami nataka kila mara niwe mwaminifu sana.

119 Sasa, ukiingia katika kanisa la Kipentekoste, jambo la kwanza . . . (Sikusudii yote. Baadhi yao huwa ni . . .) Mara nyingi unaingia katika kanisa na kuanza kuhubiri; hali ukihubiri, mtu atasimama na kuanza kunena kwa lugha. Sasa, mtu huyo mpendwa huenda amejazwa kikamilifu na Roho Mtakatifu, na huenda huyo ni Roho Mtakatifu akinena kupitia kwa mtu yule, lakini jambo ni kwamba hawajafundishwa. Kama huduma hii jukwaani imetiwa pumzi na Mungu kunena, roho za manabii humtii nabii. Ona? Mambo yote na yatendwe . . . "Sasa, fikia hapa katika Paulo mbona asema kuwa "mmoja anaponena" na kadhalika . . . "alipoingia, kulikuwa na machafuko tu."

120 Sasa, nimekuwa nikitoa mwito wa madhabahuni, na mtu fulani asimame na kunena kwa lugha. Ni . . . Vema, hata ni heri uache kutoa wito wa madhabahuni. Kunaukomesha. Ona?

121 Ndiposa, jambo lingine. Mara nyingi watu watasimama na kunena kwa lugha, na watu wameketi na kutafuna-tafuna ulimbo, wakitazama huku na kule. Kama Mungu ananena, tulia, sikiza! Kama hilo ni Kweli, kama huyo ni Roho Mtakatifu akinena katika mtu huyo, tulia kimya na kusikiza, kuwa mstarini. Huenda tafsiri ikakujia wewe. Ona? Tulia; sikiza tafsiri. Sasa, kama hakuna mfasiri kanisani, basi inapaswa watulie katika Mwili ule.

122 Ndiposa, wanaponena kwa lugha isiyojulikana, Biblia ilisema, na waseme na nafsi zao tena na Mungu. Yeye anenaye kwa lugha zisizojulikana hujifariji mwenyewe. Sasa, hizo ni lugha zisizojulikana; ndimi, lugha ni tofauti. "Hizo si kitu," yeye asema . . . Lakini kile kitoacho sauti kina maana yake. Lakini una . . . Tarumbeta ikipigwa, yakubidi ujue jinsi mlio wake ulivyo (. . . ipige tu) au hutajua jinsi ya kujitayarisha kwa ajili ya vita. Mtu ye yote akinena kwa lugha, na afanye "tuuti"; iwe hivyo tu, nani atajua la kufanya. Lakini ikipiga ya ngoma ya *kuwaamsha askari;* maana yake ni "amka!" Ikipiga *tap*, hiyo maana yake ni "ondoka." Ona? Ikipiga *shambulia* maana yake ni "shambulia." Yapaswa kuwa na maana, na si kunena tu pekee. Kwa hivyo katika kanisa, kama hakuna mfasiri, lakini kuna mfasiri, basi lugha hizo ni za kanisa.

123 Sasa, kwa swali lako, rafiki mpendwa, lisemalo, "Napenda kunena maneno elfu tano—maneno matano katika—ili watu wanielewe kuliko elfu tano (au vyo vyote isemvyo) katika lugha zisizojulikana." Hilo ni kweli. Lakini endelea kusoma . . . "isipokuwa iwe kwa ufunuo au kwa tafsiri ili iwafariji." Ona? Kufariji.

124 Sasa, nawapa tu dokezo ndogo vipi kama—vipi . . . Kama ningelikuwa mchungaji wa kanisa hili linalokuja, kama Mungu

angaliniita kuwa mchungaji wake, hivi ndivyo ningeliliendesha: Ningalijaribu kumpata kila mtu ndani humu aliye na karama. Nami ningewafanya watu hawa kukutana yapata saa moja kabla ibada haijaanza bado, katika chumba chao wenyewe. Niwaache waketi chini ya Roho. Na muda si muda, mmoja anakuja ana karama ya kunena kwa lugha. Naye anene kwa lugha. Kila mtu anatulia. Ndiposa mmoja anasimama na kufasiri yale huyu amesema. Sasa kabla hilo halijatolewa kwa kanisa, Biblia yasema sharti lipambanuliwe mbele ya mashahidi wawili au watatu. Sasa, huyo ni mtu aliye na roho wa upambanuzi (Ona?), kwa sababu wakati mwingi nguvu mbaya huingia humo. Paulo alinena habari zake. Lakini basi, nguvu za Mungu zimo humo pia. Niambie makutano ambapo uovu haumo. Niambie ambapo wana wa Mungu wamekusanyika pamoja ambapo Shetani hayuko kati yao. Ni kila kitu. Kwa hivyo usikunjie hilo uso. Ona? Shetani yuko kila mahali. Sasa, tuko hapa. Mtu fulani anena kwa lugha. Sasa, kunao watatu wanaoketi hapa walio na Roho wa upambanuzi. Na mmoja anena kwa lugha na kutoa ujumbe. Sasa, haiwezi kuwa kunukuu Maandiko, kwa sababu Mungu hapayuki-payuki, na yeye alitwambia tusifanye hivyo. Ona? Kwa hivyo si hilo. Ni ujumbe kwa kanisa.

125 Tumekuwa na vitu viwili katika ufufuo huu mpaka wakati huu. Tazama kile kila moja ilikuwa—kamilifu, kwa kila hali. Ona? Ikaingia. Mtu mmoja aliinuka, akanena kwa lugha, na kutoa tafsiri, na kurudi nyuma, na kuthibitisha ujumbe huo uliotolewa. Mwingine akainuka usiku uliopita, na kusema katika—chini ya pumzi ya unabii, na kusema kitu fulani, bila kujua yale yeye aliyokuwa akisema; ndiposa mwishowe akasema, "Heri yeye yule ajaye katika Jina la Bwana." Mara kitu fulani kilinigusa papo hapo kusema, "La, sivyo, heri yeye yule aaminiye kuwa huyu ni Bwana amekuja."

126 Ona kule—ndipo Roho Mtakatifu akashuka jengoni humu usiku uliopita. Ona? Hiyo ni kwa ajili ya kufariji. Nilikuwa nimesimama pale nikijaribu kuwaambia watu kuwa lazima wampokee Roho Mtakatifu. Na shetani alikuwa ameingia na kuwazingira watu, akisema, "Msisikize; tulieni tu."

Dada yangu alisema, "Bill, nilikuwa na furaha sana ulipokuwa ukihubiri; nilijisikia kama ningeliamka niruke na kupenya ukutani."

Nilisema, "Simama uruke." Hivyo tu.

Naye akasema, "Lakini ulipoanza kufanya hilo," kasema, "watu wakaanza kupiga shangwe," kasema, "ndipo nilijiona tu kama nilikuwa si kitu."

127 Nilisema, "Hiyo ni ibilisi. Huyo ni Shetani. Yeye aingiapo kufanya hilo," nikasema, "yakubidi usimame haidhuru." Sisi tu makuhani wa Mungu, tukitoa dhabihu za kiroho—dhabihu, matunda ya vinywa vyetu vikisifu Jina Lake. Ona?

128 Sasa, sasa, hiki ndicho kilichotendeka. Kisha Roho Mtakatifu akaingia, kwa sababu hilo lilikuwa tu. . . "Heri yule aaminiye." Usiku muwili mtatu moja kwa moja nilijaribu kusisitiza hilo ndani humu; ndiposa Roho Mtakatifu akanena na kusema (chini ya kutiwa pumzi na Mungu)—kasema, "Heri yeye yule ajaye katika Jina la Bwana." Na kabla sijasema lo lote, nilikuwa nimejirudia tena. "Heri yeye yule aaminiye Bwana amekuja katika hili." Mwaona? Na nimekuwa nikinena hili, Roho Mtakatifu ni Mungu Mwenyewe ndani yenu. Ona? Nao walikuwa wamelishika. Ona? Ndiposa Roho Mtakatifu alishuka kati ya watu. Oneni jinsi hu—hufariji, unabii.

129 Sasa, kuna tofauti kati ya unabii na nabii. Unabii unatoka kwa mmoja hadi kwa mwingine, lakini nabii anazaliwa toka utotoni nabii. Wana BWANA ASEMA HIVI. Hayo hayapambanuliwi. Huwaoni mbele ya Isaya, ama Yeremia, manabii hao wengine, kwa sababu walikuwa na BWANA ASEMA HIVI! Lakini roho ya unabii kati ya watu; yakubidi uchunguze kwa sababu Shetani atajipenyeza ndani mle. Ona? Sasa. Lakini lazima ipambanuliwe.

130 Sasa, tuta—tutakuwa na mkutano wa ufufuo. Sasa, tazama hili kwa makini sasa, ninyi wahudumu. Tunapanga mkutano wa ufufuo. Vema. Au labda sisi tuna ibada tu ya kanisa ya kawaida. Kanisa linawaka moto. Linapaswa kuwa hivyo wakati wote. Vema, labda tuna watu watano au sita walio na vipawa; mmoja anena kwa lugha, wawili au watatu labda hunena kwa lugha, wanne au watano kwa lugha, wana karama ya lugha, kunena kwa lugha. Wawili au watatu wao wanaweza kufasiri. Labda kunaye mmoja—wawili, au watatu walio na karama ya hekima. Vema. Wao wote wanakusanyika, wale watu walio na karama. . . Ninyi. . . Hizo karama hazijatolewa kwenu mzichezee, si kusema, "Mungu atukuzwe, nanena kwa lugha! Haleluya!" Una—una—unajiaibisha mwenyewe. Zimetolewa kwako kutenda kazi nazo. Na sehemu yako kanisani yabidi iwe kabla ibada yenyewe haijaanza, kwa sababu watu wajinga watakuwa kati yetu.

131 Ndipo mnaenda chumbani mle, na mnaketi mle, ninyi watu pamoja, kwa sababu ninyi ni watenda kazi pamoja katika Injili. Basi mnaketi mle. "Bwana, kuna lo lote unalotaka sisi tujue usiku huu? Nena na sisi, ee, Baba wa mbinguni," mkisali, kuomba; kuimba nyimbo. Moja kwa moja Roho anashuka, anashuka juu ya mtu fulani, ananena kwa lugha. Mmoja asimama na kusema, "BWANA ASEMA HIVI." Ni nini? Sikia. "Enda umwambie Ndugu Juma aondoke toka mahali anapoishi, kwa kuwa kesho jioni kutakuwa na kimbunga kitakachovuma nchini; na kitang'oa nyumba yake. Achukue mali yake aondoke!"

132 Sasa, hilo-hilo laonekana nzuri. Lakini ngoja kidogo. Yabidi kuwe watu watatu mle walio na Roho wa utambuzi. Mmoja

wao asema, "Ilikuwa ni Bwana." Mwingine aseme, "Ilikuwa ni Bwana." Hao ni wawili dhidi ya watatu—mashahidi wawili au watatu. Vema. Wanaandika hayo kwenye karatasi. Hivyo ndivyo Roho alivyosema. Vema. Wanaanza kuomba, wakimshukuru Bwana.

133 Kitambo kidogo, "BWANA ASEMA HIVI (nabii ainuka)—BWANA ASEMA HIVI, usiku huu, atakuja mwanamke kutoka Jiji la New York; yeye ako kwenye machela; yeye ataingia humu jengoni akiwa kwenye machela. Ana kitabaa cha kijani kichwani mwake. Anakufa kwa ugonjwa wa kansa. Kilichosababisha awe hivi, Bwana anamdai kitu—wakati mmoja yeye aliiba pesa toka kwa Kanisa Lake alipokuwa na umri wa miaka kumi na sita. Mwambie Ndugu Branham amwambie mambo haya. BWANA ASEMA HIVI, yeye akisahihisha hayo, atapona." Ngoja kidogo. Hilo laonekana nzuri sana, lakini ngoja kidogo. Utaandika jina lako kwa karatasi hii, ewe mtambuzi? Je, utaandika jina lako?

134 "Ulikuwa wa Bwana." Mmoja alisema, "Ulikuwa wa Bwana." Kisha—kisha uuandike, "BWANA ASEMA HIVI, usiku huu kutakuwako mwanamke atakayeingia, hivi na hivi." Wale walio na karama ya kupambanua roho, wawili au watatu wao wataandika majina yao. Jumbe hizo zote zimetolewa. Vema.

135 Ndipo baada ya muda mchache wanaanza kusikia kengele ikilia. Kanisa linaanza. Kisha wanaleta jumbe hizi, na kuziweka papa hapo juu ya dawati. Papa hapa ambapo zinahitajika kuwekwa. Niko mahali fulani nikisoma, nikiomba. Baada ya muda mchache naondoka baada ya nyimbo kuimbwa. Kanisa lote liko katika taratibu, watu wakiingia, na kuketi, wakitafakari, wakiomba; hilo ndilo likupasalo kufanya. Si kuja kanisani na kuongea ninyi kwa ninyi, kuja kanisani kuongea na Mungu. Fanyeni ushirika wenu kule nje. Ona? Tunashiriki na Mungu sasa. Nasi tunakuja hapa tukinena, kila kitu kimya, wastahivu, Roho akitenda kazi. Mcheza kinanda anakwenda kwenye kinanda yapata dakika tano kabla ya ibaada ya nyimbo kuanza, acheze kwa utaratibu sana:

> Msalabani sa Mwokozi,
>
> Hapo niliomba upozi, . . .

Au wimbo fulani mzuri na mtuma, kwa utivu sana. Huleta ule Uwepo wa Roho Mtakatifu mkutanoni. Ona? Vema.

136 Watu wameketi pale, Wengine wao hakika—wanaanza kulia na kuomba na kuja madhahabuni, kutubu kabla ibada haijaanza. Roho Mtakatifu yuko pale. Ona? Kanisa linaugua. Wakristo wanaomba; wako mahali pao. Hawako wameketi pale wakitafuna-tafuna peremende, wakisema, "Ewe, Bibi, nipe rangi yako ya mdomo; nataka . . . Mwajua. Mwajua. Nahitaji . . . Mwajua, majuzi nilipokuwa chini kule nikinunua vitu, nawaambieni, karibu nikanyage vidole vyenu. Je, niliwahi kuona kama hayo . . . Wawazaje kuhusu hayo?" Ee, rehema! Na

mnaiita nyumba ya Mungu. Naam ni fedheha. Mwili wa Kristo ukija pamoja. Tunaketi pale.

Mtu anayeketi karibu, "Ati, unajua tulipokuwa juu pale, huyu *fulani* na *fulani* na *fulani* . . . " Hilo ni jema nje kule, lakini ndani humu ni nyumba ya Mungu.

137 Ingia ukiomba; kaa mahali pako. Naongea sasa, si kwa makanisa yenu, ndugu. Sijui mfanyalo; nayazungumuzia maskani haya. Naongea kwa walio wangu dhahiri. Ona? Hiyo ni kweli.

138 Sasa muingiapo hivyo, muda si muda, mchungaji aondoka. Yeye ni mchangunifu. Haimpasi kujibu *hili, lile* na *linginelo*. Yeye anatoka kwe—kwenye umande wa huduma yake. Yeye amekuwa chini ya nguvu za Roho Mtakatifu. Yeye aingia ambapo ndimi zaidi za moto zimekusanyika pamoja. Karibu ni nguzo sasa (ona?) zinazunguka-zunguka. Yeye aja hapa, achukua hiki. "Ujumbe kutoka kwa kanisa: 'BWANA ASEMA HIVI, Ndugu Juma ahame nyumbani mwake. Kesho alasiri saa nane kimbunga kitaiharibu nyumba yake. Achukue vitu vyake na ahame.'" Ndugu Juma anashika hilo. Vema. Hilo, limeandikwa. "BWANA ASEMA HIVI, kutakuwako na mwanamke anayeitwa *Fulani* atakayeingia usiku huu, na ilikuwa—ametenda jambo *fulani*." (Kama vile nimekwisha sema, ona, hivyo.) Vema, hicho chawekwa pale. Ndivyo ilivyo. Wamekwisha keti mahali pao kanisani sasa. Vema.

139 Kisha yeye anachukua ujumbe ule. Na muda si muda yeye aanza kuhubiri. Hakuna kitu cha kukatiza; imekwisha tendeka. Sasa, tunaendelea. Tumehubiri ujumbe.

140 Na baada ya muda mchache wakati . . . Muda si muda ujumbe umalizikapo, mstari wa kuombea wagonjwa unaanza. Hapa yuaja mwanamke yule. Mtu fulani alinena kwa lugha na kusema yeye anakuja. Ona? Kila mmoja wetu ajua nini kitatendeka. Kila mmoja wenu ajua hilo. Oneni jinsi imani inaanza kujengeka na ndimi hizo za moto zikiwa juu yenu sasa. Yeye yuaanza kupata nafuu. Naam, ni kazi iliyomalizika; hivyo tu.

Mwanamke huyo . . . Nitasema, "Bi. *fulani,* toka Jiji la New York, anayeketi hapa . . . " Ona?

"Ee, naam. Ulijuaje hilo?."

"Ni ujumbe wa Bwana kwa kanisa. Ulipokuwa mwenye umri wa miaka kumi na sita, je, haukuwa mahali *fulani,* na ukafanya—ukachukua fedha kanisani, ukaziiba, kisha ukaondoka, ukajinunulia nguo mpya?"

"Naam, hilo ni kweli. Hilo ni kweli."

"Hayo ndiyo hasa Mungu ametwambia usiku huu kupitia kwa Ndugu *fulani,* alinena kwa lugha; Ndugu *fulani* akafasiri;, Ndugu *fulani* hapa alisema, kuhusu utambuzi, kasema ilitoka kwa Bwana. Na hilo ni kweli."

"Naam!"

"Basi, BWANA ASEMA HIVI, sahihisha hilo, na utapona kansa yako."

141 Ndugu Juma aenda nyumbani, achukua gari, arudi, achukua vyombo vya nyumbani, aondoka pale. Kesho saa nane jioni [Ndugu Branham atoa sauti kueleza—Mh.] Kitu hicho chote chaangamizwa. Ona? Ndipo kanisa latukuza . . . "Asante, Bwana Yesu, kwa fadhili zako." Sasa, hivyo ndivyo ilivyo, kujengana, kwa kanisa.

142 Basi, vipi kama haitendeki baada ya wao kuinena. Basi mna pepo mchafu kati yenu. Hamtaki huyo pepo mchafu. Mbona mwataka kitu kibaya hali a—anga zimejaa ya Kipentekoste halisi? Usichukue badilisho la kale kutoka kwa shetani. Chukua kitu halisi. Mungu anacho kwa ajili yako. Basi msiwe na mikutano mingine zaidi, na kuweka cho chote juu hapa, hata Mungu amekwisha kuthibitishia kuwa mu sahihi, kwa sababu ninyi ni wasaidizi wa kanisa katika kufanya kazi ya Injili. Sasa, mwafahamu ilivyo?

143 Na lugha—lugha zisizojulikana . . . Hakuna mtu ambaye—ajuaye yale anayonena. Yeye hunena; lakini kila sauti ina maana. Hiyo ina maana [Ndugu Branham apiga makofi—Mh.] "Glak, glak, glak!" hayo yanayo—hiyo ni—hiyo ni lugha mahali fulani.

144 Nilipokuwa kule Afrika, sikuwa nimeliamini, lakini kila kitu kilichofanya kelele kilikuwa na maana fulani. Biblia ilisema hakuna sauti isiyo na maana, isiyo na kusudi. Kila sauti inayofanywa ina maana fulani kwa kitu fulani. Naam, ningesikia watu wakisema . . . Ningesema, "Yesu Kristo, Mwana wa Mungu."

145 Mmoja wao angenena [Ndugu Branham afanya sauti kuiga mkalimani mwafrika—Mh.] Mwingine ingesema [Ndugu Branham anatoa mfano mwingine—Mh.] Na kile hayo yalikuwa ni, "Yesu Kristo, Mwana wa Mungu." Ona? Ilikuwa . . . Na isiwe na maana yo yote kwangu, lakini kwao ilikuwa ni lugha vivyo hivyo kama ninavyonena nanyi. Wakati yule mfasiri wa Zulu, Koza, Bantu, na wengineo walipofika, kila moja ya yale yaliyosemwea, kila mmoja alifahamu. Na maneno hayo mnayosikia watu hawa wakizugumza, na mnadhani ni kupayuka-payuka kwingi, sivyo; kuna maana. Kwa hivyo yatubidi kuiheshimu, kuiweka mahali pake.

146 Sasa, labda hakuna ujumbe. Sasa, ibada imekwisha; wito wa madhabahuni umefanywa. Na baada ya muda mchache mtu fulani (hakujakuwa na ujumbe nyuma kule)—mtu fulani asimama mara tu baada ya kupata nafasi. Roho Mtakatifu . . . Sasa, Biblia ilisema, "Asipokuwepo mwenye kufasiri na anyamaze." Haijalishi inajaribu kunena vipi, nyamaza.

147 Wasema, "Siwezi." Biblia ilisema unaweza. Ona? Kwa hivyo hilo—hilo latosha. Ona? Na anyamaze.

148 Kisha wakati—iwapo kila kitu kiko katika utaratibu, basi kama Roho Mtakatifu akija kwake kutoa ujumbe, basi na autoe. Hivyo ndivyo hasa jinsi yambidi mtende. Kisha tafsiri yaja, kasema, "Kuna mwanamke ndani humu anayeitwa Sally Juma (natumainia hamna mwanamke aliye na jina kama hilo, lakini . . .)—Sally Juma. (Ona?) Mwambieni kuwa huu ndio usiku wa mwisho wa kuitwa kwake. Na amkaribie Mungu kwa sababu ana muda mchache wa kuwa humu." Sasa, Sally Juma atakimbia madhababahuni upesi tu awezavyo kufika pale. (Ona?), maana huo ndio mwito wake wa mwisho. Ona? Huko ni kutoa ujumbe, au thibitisho, au jambo fulani.

149 Hilo ni kanisa la Kipentekoste likitenda kazi. Hakuna uwezekano wa pepo mchafu kupenya ndani, kwa sababu tayari . . . Biblia yasema hasa, "Hebu na iwe kwa zamu, na kwamba kwa watatu; na acha wawili ama zaidi wapambanue." Hilo ni kanisa. Lakini siku hizi tuko wapi? Kuruka, kufanya yasiyofaa, kucheka na kuendelea hali mtu fulani ananena katika lugha; mwingine akitazama, akiongea kuhusu kitu kingenecho na kukusanyika pale; mchungaji akitenda kitu fulani; au watu fulani wakikusanyika pale. Naam, hiyo si haki. Labda mchungaji anahubiri, na mtu fulani anaamka na kumkatiza katika . . . Labda kusoma Biblia na mtu fulani . . . Kusoma Biblia, na mtu fulani nyuma kule akinena kwa lugha. Ee, la! Mwaona? Mhubiri juu pale akihubiri mimbarani, mtu fulani anasimama na kumkatiza, kwa kunena kwa lugha. Ni vema. Sisemi si Roho Mtakatifu, lakini yakubidi ujue jinsi ya kumtumia Roho Mtakatifu (Ona?) kumtumia.

Sasa, ni—nachukua . . . Mna nafasi kwa moja zaidi? Basi, kesho ni Jumapili. Basi, tuta . . . Hebu tu . . . Hapa kuna moja. Nadhani ndilo lenye fadhili zaidi. Na sasa, ninyi nyote mkinivumilia kwa dakika chache tena tafadhalini. Ndiposa, nita—nawatakeni ninyi—nawatakeni ninyi mpate hili. Nililiweka hili makusudi. Hili ndilo langu la mwisho.

Sasa, kwanza, ninaenda kusoma mambo yale mawili mtu yule aliyoyauliza. Yako kwa karatasi kuukuu, yameandikwa kwa mwandiko mzuri. Sina habari huyo alikuwa nani, hakuna jina lililoandikwa kwa—kwa yo yote haya.

98. Ndugu Branham, je, ni sahihi kwa wahudumu kufanya ushawishi mkuu wa kutaka pesa katika ibada zao, wakiwaambia ya kuwa Mungu amewaambia ya kwamba watu kiasi fulani mkutanoni wanapaswa kutoa kiasi fulani? Kama hii ni halali, nataka kujua. Au kama si halali, nataka kujua. Hili limenitatiza sana.

150 Sasa, waona, rafiki, nitakwambia, nitakwambia fikira zangu. Ona? Sasa, hilo halimaanshi ni sahihi. Nafikiri ni vibaya sana.

151 Sasa, nadhani hili. Mungu alinituma nje kuhubiri. Nimeona wakati ambapo nilionekana kama kuwa ninge . . . Nami si—sikuwa na pesa kamwe. Nami ningesema, "Hebu pitisha kijisahani cha sadaka tu."

Na msimamizi angekuja na kusema, "Tazama, Billy, tumepungukiwa na dolla 5,000 usiku huu, jamani. Je, una pesa hizo Jeffersonville za kulipia?"

152 Ningesema, "Ni sawa. Mungu alinituma hapa, au singelikuja. (Ona?) Hebu pitisha tu kijisahani cha sadaka."

Na kabla mkutano huo kwisha, mtu fulani angesema, "Mwajua, Bwana aliweka moyoni mwangu kutoa dolla 5,000 kwa huu." Ona, ona? Kwanza uongozwe kulifanya.

153 Siamini katika kushawishi, na kuombaomba, na kuweka mkazo kwa pesa. Nafikiri ni jambo baya. Sasa, ndugu, iwapo hufanya hivyo, usiache nidhuru dhamiri zako. Ona? Huenda uka—ikawa umepewa kibali na Mungu kulifanya. Lakini nasema tu kujihusu mimi mwenyewe. Siamini hiyo.

154 Sasa, hata najua wahudumu waendao na kusema . . . Nilisimama—si muda mrefu uliopita . . . Sasa, hii si Wapentekoste, hii ni . . . Vema, ni makanisa (ona?), makanisa mengine. Ilikuwa katika mkutano mkumwa wa kampi. Gertie, ulikuwa pamoja nami, wengiene wengi walioko. Nao walichukua alasiri nzima kwenye dhehebu maarufu—mawili au matatu yayo pamoja (hayo ni makanisa ya kawa—kawaida, kama makanisa yetu ya kisasa hapa mjini, na mengineyo) kwenye mkutano mkubwa— nao walichukua alasiri nzima, wakisimama jukwaani na kutisha kuwa—kuwa Mungu angeharibu mimea yao, angewaambukiza watoto wao ugonjwa wa kuupooza, na mengineyo kama hayo, kama hawangechanga katika mkutano huo. Hilo ni kweli hasa, huku Biblia ikiwa mbele yangu. Nilisema, "Ni kumkufuru Mungu na wafuasi Wake." Kama Mungu amekutuma, yeye atakushughulikia. Kama Yeye hajakutuma, basi na dhehebu lile likutumikie. Lakini— lakini wewe . . . Mungu akikutuma, Yeye atakushughulikia.

99. Vipi kuhusu mchezo wa Krismasi katika kanisa la Roho Mtakatifu?

155 Vema, kama ni kuhusu Kristo, huenda ikawa sawa. Lakini kama inahusu Baba Krismasi, simwamini huyo. Nime—nimekwisha ni—nimekwisha kuyaacha hayo. Siamini katika Baba Krismasi kamwe. Ona? Na baadhi ya hivi vitu vidogo vya Krismasi walivyo navyo, nadhani ni upuzi. Na . . . Lakini naona wamemwondoka kabisa Kristo katika Krismasi na kumweka Baba Krismasi mle.

156 Na Baba Krismasi ni hadithi ya kubuniwa tu. (Natumaini siudhi dhamiri zenu, kuhusu watoto.) Lakini nitawaambia. Hapa muda mchache uliopita, yapata miaka ishirini na mitano, au thelathini iliyopita, wakati mhudumu fulani hapa

mjini, mchungaji wa—wa kanisa fulani kubwa hapa mjini, niliyemjua vema sana, rafiki msiri wangu, alinijia. Na Charlie Bohannon (Ndugu Mike, unamkumbuka Charlie Bohannon, rafiki yangu mwema). . . Aliketi pale afisini mwake na kusema, “Sitawaambia kamwe watoto wangu au kuruhusu wajukuu wangu waambiwe uongo huo tena.” Yeye alisema, “Mtoto wangu mvulana alinijia alipopata umri wa miaka kumi na miwili, na akinena kuhusu Baba Krismasi.” Naye alisema, “Naam . . . Mpendwa nataka kukwambia jambo fulani,” kasema, “Mama . . . ” Wajua, na kuendelea kumwambia yale yeye alifanya.

Ndipo aliporudi, kasema, “Basi, Baba, je, huyu Yesu ni kitu kile kile.”

157 Mwambie kweli. Baba Krismasi ni ubuni wa Katoliki kuhusu mtu fulani, Kriss Kringle au Mtakatifu Nichola, maskini Mjerumani Mkatoliki mtakatifu wa kale aliyezunguka huku na huko akiwatendea mema watoto. Nao wameifuatilia kote kama mapokeo. Lakini Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu. Yeye ni halisi, na yu hai.

Sasa, hapa kuna swali, la mwisho, ambalo ni . . .

158 Sasa tazama. Huenda usikubaliane nami kwa hilo. Lakini usipokubaliana nami kumbuka, hebu na tuwe marafiki, utafanya hivyo? Nawapenda ninyi nami sitaki ku—kuwaudhi. Ni—ninataka tu kuwa mwaminifu. Kama siwezi—nikimwambia mvulana wangu uongo, basi mimi ni mwongo. Ona? Nataka kumwambia kweli.

159 Sasa, namwambia kuhusu Baba Krismasi, namwambia “Naam, hakika, kuna Baba Krismasi. Mtazame Baba huyo usiku wa Krismasi.” Ona? Naam.

160 Mwajua, hivi majuzi nilikuwa chini kule, nami nilijaribu hilo kwa msichana mdogo ili nione tu. Niliyajuta hivi majuzi jengoni. Nao walikuwa wamesimama pale, pale chini kwa Quaker Maid. Nami nikaenda kule kununua vitu vya nyumbani. Na kwa hivyo sisi, mimi na mke wangu tulikuwa ndani mle. Na kulikuwa na msichana mdogo, hakuwa na umri unaozidi miezi kumi na minane, naye alikuwa amesimama pale akizunguka—akiimba, “Kengele Inalia, Kengele Inalia . . . ” Nami nilisema . . . Katika kituo chake kidogo, mwajua, ameketi nyuma ya gari ndogo la kukokotwa.

Nilimuuliza, “Je, unamtafuta Baba Krismasi?”

Yeye alisema, “Huyo ni baba yangu, Bwana.”

Nilisema, “Heri maskini moyo wako, Kipenzi. Una hekima.”

Sasa, hapa kuna moja gumu sana, marafiki. Na katika hili . . . Ndipo nitafunga. Ee, ni—ni Andiko tamu, lakini yaonekana ni gumu kwa kila mtu. Na lilinitatiza sana kwa miaka na miaka; na ni kwa neema ya Mungu pekee . . . Na mke wangu

mpendwa, anayeketi nyuma pale sasa, yeye aliposikia kuwa nina swali hilo alasiri hii, yeye alisema, "Bill, utajibuje hilo?" Akasema, "Kila mara mimi mwenyewe nimeshangaa kuhusu hilo." Kasema, "Singewahi kulifahamu." Kisha akasema . . .

Nilisema, "Njoo usiku huu, mpenzi. Nitafanya niwezavyo kwa msaada wa Mungu."

100. Ndugu Branham, tafadhali fafanua Waebrania 6:4 mpaka 6.

161 Hilo wakati mmoja hakika lilini . . . Ona, sasa inakubidi utazame hapa kwa imani yako, neema, usalama wa waamini—uvumilio wa watakatifu, samahani, uvumilivu wa watakatifu. Waebrania sura ya 4 mpaka 6.

Sasa, mara tu—tumalizapo hili, basi natumai Mungu atanisaidia kulifanya lote dhahiri kwenu. Nasikitika, ni—nina ujumbe usiku huu; labda nitahubiri kitu kile kile asubuhi kwenye—kwenye ibada. Ndipo nitaondoka.

162 Sasa, hili ni gumu kabisa. Ona? sasa, yakubidi uchunguze. Sasa kumbuka, tunaamini na kufundisha kwenye kanisa hili, si kuwa kila kitu kinachoinuka na kupaza sauti, kila kitu kinenacho katika lugha, kila kitu kisalimianacho kwa mkono na mhubiri, kina Uzima wa Milele. Lakini tunaamini kama una Uzima wa Milele, kama Mungu amekupa Uzima wa Milele, unao milele. Ona? Kwa sababu tazama. Kama sivyo Yesu ame—amekuwa mwalimu wa uongo. Katika Yohana Mt. 5:24, Yeye alisema, "Yeye alisikiaye Neno Langu na kumwamini Yeye aliyenipeleka yuna Uzima wa Milele, wala haingii hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani." Sasa bishana naye. "Wote alionipa Baba . . . Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu. (Ninanukuu Maandiko.) Wote wajao Kwangu . . . Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa ba Baba Yangu kwanza. Na wote alionipa Baba watakuja kwangu. (Ona?) Na wote wanijiao, nitawapa Uzima wa Milele (Yohana Mt. 6), Nami nitamfufua siku ya mwisho." Hayo ni maneno Yake.

163 Sasa tazama. Kama ningerudi katika Waefeso sura ya 1, Paulo akihubiri . . . Sasa, Wakorintho, kila mmoja alikuwa na lugha na wimbo. Mwatambua makanisa mengine hayakuwa na shida hiyo. Yeye hakusema lo lote kuhusu hilo. Je yeye alitaja lugha mahali po pote katika kanisa la Efeso, kanisa la Warumi? La! Walikuwa na lugha na kila kitu kama tu vile Wakorintho walivyokuwa nazo, lakini walikuwa wameiweka katika utaratibu. Wakorintho walishindwa kuiweka katika utaratibu. Ona? Lakini Paulo alishuka akaenda kule na kuliweka kanisa lile katika utaratibu.

Sasa yeye . . . Naamini, kama asemavyo Oral Roberts "Mungu ni Mungu mzuri." Je si mnaamini hilo?

164 Na unasema, "Vema, na Wapentekoste, je, wenye lugha basi, Ndugu Branham?" Nadhani walipata Roho Mtakatifu. Hakika walipata. Vema, mbona? Tazama. Je mwaamini Yeye ni Mungu mzuri? Tomaso alisema wakati mmoja, "Wajua, Bwana . . . "

Wengine wote walimwamini Yeye. Kasema, "Ee twajua Yeye ni halisi!"

"Ee," Tomaso alisema, "la, la, siamini. Njia pekee nitakayoamini, itanibidi niwe na ishara fulani. Itanibidi niweke kidole changu ubavuni Mwake na katika alama ya misumari mikononi Mwake."

Yeye ni Mungu mzuri. Yeye alisema, "Njoo, Tomaso. Ndiyo hii."

"Ee," Tomaso alisema, "sasa naamini."

165 Yeye alisema, "Naam, Tomaso, baada ya kuniona Mimi, na kunigusa, na kuweka mkono Wangu—mikono yako ubavuni Mwangu, unaamini. Lakini zaidi vipi ilivyo zawadi yao ambao hawajaniona bali wanaamini." Yeye ni Mungu mzuri. Yeye hukupa wewe hamu ya moyo wako, hakika. Hebu tumwamini Yeye tu. Hilo ni—hilo ni—hilo ndilo pigo la mauti kwa Shetani. Mtu anapoamini Neno la Mungu, ndugu, hilo litamuua Shetani kila wakati. Hilo ndilo pigo kuu zaidi Shetani awezalo kulipata, mtu anapoamini Neno analosema Mungu. Kama nilivyosema, "Mtu hataishi pekee (Yesu, usiku uliopita), bali kwa kila neno litokalo . . . "

166 Sasa, tazama hili. Sasa nitaanzia kwa kifungu cha kwanza:

> *Kwa sababu hiyo, tukiacha kuyanena mafundisho ya kwanza ya Kristo, tukaze mwendo ili tuufikilie utimilifu;* . . . (Sasa, jambo la kwanza nawatakeni ninyi mjue: Paulo anazungumzia nani hapa? Waebrania; wao husema ni Waebrania, waliofundisha Kitabu cha Waebrania. Sivyo? Wayahudi waliokuwa wamemkataa Yesu . . . Je, mwaweza kulifahamu sasa? Yeye anawazungumzia Wayahudi, akiwaonyesha wao kuwa kile kivuli cha torati ni mfano wa Kristo. Vitu vyote vya kale ni mfano wa vile vipya. Sasa tazama.)
>
> . . . *tukiacha kuyanena mafundisho ya kwanza ya Kristo, tukaze mwendo ili tuufikilie utimilifu;* . . .

167 Sasa, yeye amekuwa akiwaambia kuhusu mafundisho. Hebu tuende tukaongee kuhusu vitu vilivyotimilika. Sasa, umekamilika katika Mungu unapotiwa muhuri na Roho Mtakatifu hata siku ya ukombozi wako. "Kila aliyezaliwa na Mungu (1 Yahana) hatendi dhambi; hawezi kutenda dhambi, kwa sababu Uzao wa Mungu wakaa ndani yake."

168 Mtu aliyejazwa na Roho Mtakatifu, si yule adhaniye amejazwa, lakini yeye aliyezaliwa na Roho wa Mungu hatendi dhambi, kwa kuwa Uzao wa Mungu uko ndani yake, naye

hawezi kutenda dhambi. Ona? Je, Biblia inasema hilo? Kwa hivyo ndivyo ilivyo. Wewe una. . .Si kile unachotenda, kile—ni kile—si kile ulimwengu unachowaza kukuhusu wewe, ni kile Mungu anachowaza juu yako. Ona, ona? Huwezi. . .Nawezaje kuwa na amri iliyoandikwa na mkuu wa mji, kuwa naweza kuendesha gari maili arobaini kwa saa mjini, kisha askari ye yote anishike? Siwezi. Nawezaje kutenda dhambi hali kuna toleo la damu mbele ya Mungu kila mara ambapo Yeye hata hawezi kuiona, wakati kuna kinga kwenye—kwenye—mbele yangu na Mungu, ngao ya Damu; maana tumekufa na uhai wetu umefichwa pamoja Kristo katika Mungu, kutiwa muhuri na Roho Mtakatifu. Inawezekanaje kamwe wewe kutenda jambo mbaya machoni pa Mungu. "Tukitenda dhambi kusudi (Waebrania 10) baada ya kuupokea ujuzi wa Kweli, hakuna tena dhabihu ya dhambi." Ndani humu haiwezekani (ona?) kutenda dhambi kusudi.

169 Sasa, hebu tuendelee na kusoma. Vema

> *. . .utimilifu, tusiweke msingi tena wa kuzitubia kazi zisizo na uhai, na. . .imani kwa Mungu,*
>
> *Na wa mafundisho ya mabatizo, kuwekea mikono, na kufufuliwa wafu, na. . .hukumu ya milele.*
>
> *Na hayo. . .tutafanya Mungu akitujalia.*
>
> (Sasa hapa Ndipo walipotaka tuanzie toka kwa kifungu cha nne.) *Kwa maana hao waliokwisha. . . kupewa nuru na kukionja kipawa cha mbinguni, na kufanywa washirika wa Roho Mtakatifu,*
>
> *Na kulionja neno zuri la Mungu, na nguvu za zamani zijazo,*
>
> *Wakaanguka baada ya hayo, haiwezekani kuwafanya upya—upya tena hata wakatubu; kwa kuwa wamsulubisha Mwana wa Mungu mara ya pili kwa nafsi zao, na kumfedhehi kwa dhahiri.*

170 Sasa, sasa, hilo laonekana kama, jinsi unavyosoma pale, kuwa mtu anaweza kumpokea Roho Mtakatifu, ndiposa aanguke na apotee. Lakini haiwezekani kwake kufanya hivyo. Ona? Haiwezekani kwao waliokwisha kupewa nuru. Sasa, tazama hapa. Yeye ananena na nani? Yeye ananena na hao Wayahudi waliokwamia mpakani. Yeye hakusema kuhusu mtu aliyejazwa na Roho Mtakatifu; yeye alisema, "Kama yeye amekwisha kulionja Neno la Mungu."

171 Sasa, hebu nitoe mfano, ili muone na hamtaikosa sasa. Sasa, yeye anawaandikia hawa Wayahudi. Wengine wao ni waamini wakwamia mpakani. Ona? Yeye alisema, "Sasa tutaacha kazi hizi tukanene kuhusu utimilifu." Kasema, "Sasa, tunaongea kuhusu mabatizo, na ufufuo wa wafu, na kuwekea mikono, na kila kitu; lakini hebu tuendelee mbele sasa kuongea

kuhusu utimilifu. Sasa, tutaongea kuhusu uingiapo katika Roho Mtakatifu. Sasa, umekuwa mkutanoni vya kutosha . . . "

172 Nanyi mmewaona watu hao. Watasimama karibu; nao hawataingia ndani wala kutoka nje. Wanafurahia Roho Mtakatifu. Watajongea karibu. Na labda Roho Mtakatifu afanye kitu fulani na—jamani, wataamka na kupiga shangwe, na kuruka juu chini sakafuni, lakini wao wenyewe hawataki kamwe kumpokea. La, la! Ona? Nao watasema, "Ee, naam, hilo ni zuri. Ee, sijui kuhusu hilo sasa." Ona, ona, ona? Waamini wakwamia mpakani. Karibu sana hadi wao wanaweza kumuonja, lakini hawampokei. Ona? Sasa, wanakaa karibu hivyo sana hata baada ya muda mchache wao wanachukuliwa mbali kabisa. Naweza kutaja majina ya wengi waliokuwa maskanini, waliotenda jambo lile lile. Wakaanguka tena, kuwafanya upya tena hata wakatubu, hakuna toba kwao. Wao walimhuzunisha tu Roho akaondoka kwao. Wamekuwa karibu sana hata . . .

173 Hapa, mkifungua pamoja nami (hamna wakati, najua, sasa) lakini kama mngefungua Kumbukumbu la Torati sura ya 1 na kuisoma, mtapata jambo lile lile. Mkiiandika sasa, Kumbukumbu la Torati sura ya 1. Sasa, na mwazie kifungu cha 18 na kusoma hadi cha 26. Kumbukumbula Torati . . . mtaona . . . Sasa tazama. Israeli yote . . . Yale watu hao walifanya, walikuja hadi Kadeshi-barnea. Ee, naona kitu fulani! Maskani haya, huu ulimwengu wa Kipentekoste uko Kadeshi-barnea hivi sasa. Naam, hasa, Ndugu Neville. Tuko Kadeshi-barnea, kwenye hukumu ya ulimwengu (ilikuwa kiti cha hukumu).

174 Na wapelelezi walienda. Yoshua alisema hapa, "Sasa, naliwatuma wapelelezi . . . "—au Musa, samahani, "Naliwatuma wapelelezi—kumi na wawili—mmoja, wao—mtu moja toka kwa kila kabila lenu. Naliwatuma wapeleleze nchi ile na walete habari." Sivyo?

Na waliporudi, kulikuwa na tisa kati ya kumi na wawili kasema, "Ee, ni nchi njema, lakini ee, jamani, hatuwezi kuitwaa. Loo masalale! Waamori wako humo, nasi twaonekana kama mapanzi kando yao. Wao wana silaha. Kuta zao ni kubwa. Mama wee! ni—mbona, afadhali tungelikufia kule Misri badala ya kutuleta hapa."

175 Mbona, maskini Kalebu na Yoshua wakainuka pale na kuwatuliza; kasema, "Sisi twaweza kushinda bila shaka." Naam, bwana! Mmoja ndiye huyo. Sasa tazama. Nini kilitendeka? Kalebu na Yoshua walijua kuwa Mungu alitoa ahadi hiyo: "Sijali ni kubwa vipi, pingamizi ni kubwa vipi, wao ni warefu vipi, wao ni wakuu jinsi gani, hilo halifai kitu. Mungu alisema hivyo, nasi tunaweza kuitwaa." Na mwajua wao walikuwa ndio tu watu wawili ambao—kati ya hao milioni mbili na nusu waliowahi kuvuka na kuingia katika nchi hiyo? Kwa sababu walishikilia imani yao katika yale Mungu alisema kuwa ni Kweli. Amina!

176 Maskani haya, hivi sasa yanasimama pale Kadeshi-barnea. Tazama, watu hao walikuwa karibu sana hata walionja zabibu toka kwa nchi ile. Walikula zabibu. Wakati Kalebu na wengineo walipovuka na kuleta zabibu, watu hao walitwaa kadha na kuzila. "Ee, hizo ni nzuri lakini hatuwezi kufaulu." "Wale walioonja kazi nzuri za Mungu, wamekwisha kuonja Roho Mtakatifu, wakaona uzuri Wake, wakamwoja, wameonja Neno la Mungu. . . " Ona hilo? Hakuna ye yote wao, hamna hata mmoja wao aliyeruhusiwa kuvuka. Waliangamia nchini mwao juu hapa jangwani. Wao hawakuvuka kamwe, bali walikuwa karibu kutosha hata kuionja, lakini bila neema na imani ya kutosha kuitwaa. Ndivyo ilivyo.

177 Sasa, sasa sikia huyo mtu mpendwa aliyeandika hili. Hebu tusome tu kifungu kinachofuata. Chunguza hicho kwa dakika moja hivi. Mtazame Paulo. Sasa hebu tusome cha 7:

> *Maana nchi . . . inayoinywa mvua inayoinyeshea mara kwa mara, na kuzaa mboga zenye manufaa kwa hao ambao kwa ajili yao yalimwa hushiriki baraka zitokazo kwa Mungu;*
>
> *Bali ikitoa miiba na magugu hukataliwa na kuwa karibu na laana; ambayo mwisho wake ni kuteketezwa.*

178 Sasa, oneni yale yeye anasema. Sasa tazama. Kulikuwa na swali hili hapa; sasa, ndiposa tutafunga . . . Kitu hiki kilikuwa karibu kuniva kwa miaka mingi.

179 Nilihudhuria mkutano wakati mmoja ambapo watu walikuwa wakinena kwa lugha kule Mishawaka, Indiana. Sasa, niko mbele ya kundi langu mwenyewe. Mmewasikia watu wale—mmenisikia nikisimulia hadithi ya maisha yangu, na kuhusu yule mtu mweusi aliyesema, "Yeye yuko hapa. Yeye yuko hapa." Sasa, nilisimulia hayo.

180 Lakini yaliyosalia: niliwaona watu wawili. Walikuwa . . . Mmoja angetoa ujumbe, mwingine angefasiri. Mmoja akatoa ujumbe, na mwingine akafasiri. Na ndugu, walikuwa sahihi. Hivi tu . . . Niliwaza, "Jamani! Sijapata kuona cho chote kama hicho." Nilisema, "Niko kati ya malaika." Niliwaza, sijawahi kuona lo lote . . . Mmoja angenena, na mwingine . . .

181 Nami niliketi pale na mhudumu mzee, mwajua [Nafasi tupu kwenye ukanda—Mh] . . . watu wote na wakati mwingine na kusalimiana nao kwa mikono. Sikuwahi kuwaona watu kama hao maishani mwangu. Wangenena ujumbe na mwingine angefasiri. Loo, masalale! Ilikuwa ya ajabu! Mmoja angenena na mwingine angefasiri. Wote wawili . . . Nao wangegeuka kuwa weupe kama chokaa walipoinua mikono yao juu. Nilidhani, "Ee loo, jamani, nimekuwa wapi maishani mwangu mwote. Hili ndilo jambo!" Nilisema, "Lo, Pentekoste wako sahihi." Naam hasa.

182 Sikuwa nimewahi kuona mengi ila tu yaliyokuwa humu karibu, ambako wale—labda wanawake kama wawili hivi

kwenye misheni mahali fulani. . . Nao wangekuwa wakizozana; na mmoja akimwita mwingine "Mwewe anayeatamia," na mwajua, hivyo tu, wakizozana wao kwa woa. Si kudharau wanawake sasa au ye yote, bali tu. . . Ilikuwa katika udhaifu. Kama ye yote wenu. . . Wakumbuka, Ndugu Graham. Ulikuwa tu mvulana mdogo wakati huo. Na kwa hivyo, hivyo ndivyo ilivyokuwa. Basi nilisikiza hayo, nami nilidhani, "Jamani, nimewafikia malaika."

183 Siku moja nilipofika pembeni mwa nyumba yapata siku ya pili, nilikutana na mmoja wa watu wale. Nikasema, "U hali gani, Bwana?"

Akasema, "Njema." Yeye alisema, "U—jina lako nani?"

Nilijibu, "Branham."

Yeye akauliza, "Unatoka wapi? Hapa?"

Nami nilisema, "La, mimi natoka Jeffersonville."

Akasema, "Vema, hilo ni jama. Wewe u Mpentekoste?"

Nikasema, "La bwana, mimi si Mpentekoste." Nilisema, "Sikubaliani na njia ya Pentekoste ya kumpokea Roho Mtakatifu," nilisema, "ingawaje," nilisema, "niko hapa kujifunza."

184 Yeye alisema, "Vema hilo ni zuri sana." Na nikiongea naye nikashika roho yake (kama yule mwanamke kisimani), yeye alikuwa Mkristo halisi. Ndugu, nakusudia yeye alikuwa mstahivu. Yeye alikuwa mzuri. Sasa, ninyi nyote. . . Wangapi wamekuwa katika mikutano yangu na mambo hayo yakatendeka? Mwaona? Na mtu yule alikuwa mkamilifu kabisa. Kwa hivyo, ni—nilidhani, "Pale! Lo, ajabu vipi!"

185 Yapata jioni, alasiri wakati fulani, nilikutana na yule mwingine. Nilisema, "U hali gani bwana?"

Yeye akaitikia, "Njema. Jina lako nani?" Nikamwambia. Naye akasema, "Ume. . . U—wewe u Mpentekoste?"

Nikasema, "La, bwana, si Mpentekoste hasa, sidahani." Nilisema, "Niko tu hapa tu kujifunza."

Alisema—nikasema—akasema, "Umewahi kumpokea Roho Mtakatifu?"

Nikasema, "Si—sijui." Nilisema, "Kulingana na jinsi ninyi mliye naye, nadhani sijampokea."

Naye akasema, "Umewahi kunena kwa lugha?" Nikasema, "La, bwana!"

Yeye akasema, "Basi hujampokea."

186 Nami nikasema, "Vema, na—nadhani hiyo ni kweli" Nikasema, "Sijui. Nimekuwa nikihubiri kwa miaka isiyozidi miwili," nami nikasema, "Sijui habari zake sana." Nilisema, "Labda sijui." Nilisema, "Siwezi kufahamu. . ." Jambo ni

kwamba, nilikuwa nikijaribu kumshikia pale (ona?), kuishika. Na nilipofanya hivyo, kama nimewahi kukutana na mnafiki, huyo ni mmoja wao. Mke wake alikuwa na nywele nyeusi; naye alikuwa akiishi na mwanamke mwenye nywele nyeupe za shaba, alikuwa amepata watoto wawili kwake; huku akinena kwa lugha, akizifasiri tu kamili kama ziwezavyo kuwa. Nami nikasema, "Sasa, Bwana, niko wapi?" Toka kwa malaika, sikujua nilikuwa wapi tena. Nikasema, "Mi—mi—mimi ni wa kimsingi; haina budi kuwa katika Biblia. Yabidi iwe sahihi. Kuna kasoro fulani mahali fulani, Bwana. Yawezekanaje?"

187 Niliingia mkutanoni usiku huo, na Roho yule angeshuka; na ndugu, ungesikia mguso Wake! Na ilikuwa ni Roho Mtakatifu. Naam, Bwana! Kama haikuwa, ilishuhudia pamoja na roho yangu kuwa ilikuwa ni Roho Mtakatifu. Nami nilikuwa tu mhubiri mchanga, na sikujua jinsi—mengi kuhusu roho wa utambuzi. Lakini nilikuwa ninaketi pale. Nami nalijua Mungu yule yule aliyeniokoa, huko kulikuwa kujisikia kule kule... Nilijisikia kama nilikuwa napitia katika dari, kulikuwa ni kujisikia kwa ajabu katika jengo hilo. Nami nilidhani...

188 Kulikuwamo watu wapatao 1500? Nami niliwaza, "Lo, jamani, lo! Vikundi viwili au vitatu vyao vilikuwa vimekusanyika pamoja. Nami niliwaza, "Aisee, jamani! Yawezekanaje? Sasa, huyo Roho mkuu katika jengo hili akishuka hivyo; na hapa, tazama haya yanayoendelea juu pale, wao watu wakinena kwa lugha, kutafsiri, kutoa ujumbe kikamilifu—na mmoja awao ni mnafiki na mwingine mtu halisi wa Mungu." Nami nilidhani, "Sasa, nimetatanishwa. Sijui la kufanya."

189 Vema, mara tu baadaye, rafiki wangu sana, Ndugu Davis (mwajua), alianza kusema mimi nilikuwa mwana serere. Huyo ni kitu cha kuchezea cha msichana, mwajua. Na kwa hivyo... Nilikuwa sijaoa. Na kwa hivyo mimi... Yeye alianza kunitendea mabaya, ndiposa akaendelea, kunifanyia mzaha.

190 Nasi tulikuwa na... Na mama yako nasi sote tulikuwa na mikutano midogo tofauti mahali mbali mbali. Maskani haya haya—hayakuweko wakati huo, nasi tulikuwa na mikutano midogo mahali mbali mbali. Na hatimaye siku moja, baada ya maskani haya kujengwa, miaka mingi baadaye, nilienda kule Green's Mill kwenye pango langu kuomba kwa sababu Ndugu Davis alikuiwa amesema mambo mabaya sana kunihusu mimi katika lile—katika—katika gazeti lake. Nilikuwa nampenda. Sikutaka cho chote kitendeke, nami—nilienda juu pale kumwombea. Nami nikakwea kule, na kuingia pangoni mle. Nami nilikaa ndani mle kwa karibu siku mbili. Nilisema, "Bwana, umsamehe. Yeye—yeye hakusudii—hakukusudia hilo." Nami niliwaza, "Mwajua..." Nilikumbuka tu Andiko fulani.

191 Nami nikatoka nje na kulikuwa na gogo (gogo lile lingali pale, lilikuwa hapo muda mchache uliopita) chini ya mlima

na kukingama kijia kitokacho kwenye ghuba ndogo. Nami nikatagaa kwenye gogo lile, nikatazama hapa na pale kote milimani nyuma—nyuma kule, na kuweka Biblia yangu hivyo. Niliwaza, "Mwajua . . . " Nilikuwa nawaza kuhusu Andiko fulani: "Yule mfua shaba alionyesha ubaya mwingi kwangu, na kusema mambo." Mwajua . . . niliwaza, "Naamini nitasoma tu hayo." Nikafungua Biblia, na kusema, "Vema . . . " Nikapangusa uso wangu, na upepo ukavuma, ukafungua Waebrania 6. "Vema," nilisema, "hapo sipo yaliko." Nami nikairudisha hivi. Na upepo ukavuma tena na kuirudisha pale tena. Nami nilisema, "Sasa, ajabu hii, upepo kuvuma kuirudisha hivyo." Kwa hivyo niliwaza, "Vema, naamini nitaisoma." Nayo ikasema:

> *Kwa maana haiwezekani kwa hao waliokwisha kupewa nuru; kufanywa washirika wa Roho Mtakatifu, na kulionja . . . Neno zuri la Mungu, na nguvu za zamani zijazo.*

Niliwaza, "Vema, sioni lo lote kwa hilo." Kasoma kuendelea, sura inayofuata. Hamna kitu humo. Nilisema, "Vema, hiyo—hiyo imetosha kabisa." Nami—nikaiona hivi, na ikarudi tena. Nami nikaichukua, kisha nikawaza, "Vema nini hiyo?" Nikaendelea kuisoma, na kuisoma, na kuisoma. Nikasema, vema, siwezi kufahamu." Ndipo nikaendelea . . . Nami nikaendelea kusoma:

> *. . . haiwezekani kwa waliokwisha kupewa nuru . . .*

> Ilifikia chini hapa mahali fulani hapa ambapo ilisema:

> *Maana nchi . . . inayoinywa mvua inayoinyeshea mara kwa mara, na kuzaa mboga zenye manufaa kwa hao ambao kwa ajili yao yalimwa, hushiriki baraka zitokazo kwa Mungu;*
>
> *Bali ikitoa miiba na magugu hukataliwa na . . . kuwa karibu na laana; ambayo mwisho wake ni kuteketezwa.*

192 Nikasema, "Nashangaa maana ya hayo?" Ninge . . . Sasa, sikuwa nawaza kuhusu lo lote juu pale. Mara . . . Na mara nilipokuwa nimeketi pale, nilidhani Bwana angenipa ono kuhusu Ndugu Davis na wengine kule. Nami nilikua nimeketi pale; nikatazama, kisha nikaona kitu fulani kikizunguka karibu na hicho kitundu mbele yangu. Na ilikuwa ni dunia ikizunguka. Nami nikaona ilikuwa imevunjwa-vunjwa, ilionekana kama yote ilikuwa imelimwa. Na Mtu mmoja aliondoka akiwa na chombo kikubwa m—m—mno mbele Yake kilichojaa mbegu, na Yeye alikuwa akipanda mbegu kote kote duniani alipokuwa akienda. Kisha akaenda kupita mpindo wa dunia hata sikumwona tena. Na mara tu Yeye alipotoweka machoni pangu, hapa kukaja mtu aliyeenda kifichifichi, amevalia mavazi meusi, akienda huko hivi, akienda [Ndugu Branham atoa sauti kuotoa mfano—Mh.] akipanda mbegu mbaya [Ndugu Branham arudia sauti ile—Mh.] Nami nikayatazama hayo, na dunia ilipozidi kupinduka . . .

193 Kitambo kidogo ngano ikaota. Na wakati ngano ilipoota, toka mle kukaota mbigili, na mibaruti, na miiba, na magugu yanukayo, na kila kitu kikiota, makwekwe, na kila kitu kikikua katika ngano ile. Na vyote vilikuwa vikimea pamoja. Na kukaja ukame mbaya sana, na zile ngano ndogo zikainamisha vichwa vyao hivyo, kisha maskini mbigili ndogo na mbaruti, na miiba, vikainamisha vichwa vyao. Kila gugu liki-[Ndugu Branham afanya sauti ya kutweta—Mh] pumua hivyo. Ungevisikia tu. Nazo zilikuwa zikiomba zipate mvua, mvua.

194 Na baada ya kitambo kidogo, kukaja wingu kuu mno, na maji yale yakabubujika aradhini. Na iliponyesha mle, ngano hiyo ikaruka juu na kuanza kupaza sauti, "Utukufu, Haleluya, Bwana asifiwe!" Pale maskini ule mche wa magugu yanukayo ukaruka na kupaza sauti, "Utukufu, Bwana asifiwe, Haleluya!" Miiba na mingine yote ikicheza hapa na pale shambani ikipaza sauti, "Utukufu, Haleluya, Bwana asifiwe!"

Vema, nilisema, "Siwezi kufahamu hilo."

195 Ono lile likaniacha; ndipo nilirudia hayo tena: "Magugu hukataliwa . . . " Ndipo nikafahamu. Ile . . . Yesu alisema, "Mvua huwanyesha wenye haki na wasio haki" Mtu anaweza kuketi mkutanoni, aweza kunena kwa lugha, aweza kupiga shangwe na kutenda kama tu wengine wao wote akiwa na Roho Mtakatifu halisi na bado asiwe katika Ufalme wa Mungu. Hilo ni sawa hasa. Si Yesu alisema, "Wengi watasimama siku hiyo na kusema, "Bwana, 'sikutoa pepo kwa Jina Lako; sikutabiri (kuhubiri) kwa Jina Lako; sikufanya kazi nyingi kuu kwa Jina Lako?" Yesu akasema, "Ondokeni Kwangu, ninyi mtendao maovu, sikuwajua ninyi kamwe." Na hiyo je?

196 Maana yake halisi ndiyo hii. Ona? Walionja mvua nzuri toka Mbinguni. Lakini kwanza, walikuwa wamekosea. Tangu awali kusudi zao hazikuwa safi; shabaha zao hazikuwa safi. Hilo . . . Huwezi kueleza ile . . . Mwajua, katika mavuno yeye alisema, "Niende nikayang'oe yote?"

197 Yeye alisema, "Viacheni vyote vikue pamoja, na kwenye siku hiyo hii miiba na magugu vitateketezwa pamoja, na ngano itakusanywa ghalani." Sasa, utajuaje ipi ni miiba, au ipi ni gugu, au ipi ni ngano? "Kwa matunda yao mtawajua." Mwaona, Ndugu, Dada, mti mzuri hauwezi kuzaa tunda baya. Haijalishi, mahali fulani njiani, utajuta. Kwa hivyo, wewe katika kutafuta ubatizo wa Roho Mtakatifu . . . Nina furaha kwa ye yote aliyeandika hilo. Ona?

198 Sasa, hao waamini wakwamia-mpakani nyuma kule, walikuwa pamoja nao hasa. Walitahiriwa kwa tohara yao. Walienda hata kwenye nchi ambayo Mungu aliahidi, hadi ukingoni mwayo. Mara nyingi watu wengi hutembea hadi ukingoni huo. Yeye atatembea hadi kufikia ubatizo wa Roho Mtakatifu na kuukataa. Yeye hataki kujitolea. Yeye atafika

moja kwa moja kwenye ubatizo wa Kimaandiko katika Jina la Yesu Kristo na kuupa kisogo, na kukataa hata kuuona.

199 Hakuna Andiko hata moja katika Biblia nzima ambapo mtu ye yote aliwahi kubatizwa kwa jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu, si hata Andiko moja. Kanisa Katoliki lilivanzisha, ukapitia kwa Luther, ukaingia kwa Wesley, na umeendelea hata hapa. Hilo ni sawa hasa. Lakini utaratibu wa Kimaandiko ni Jina la Bwana Yesu Kristo. Huo ndio ubatizo wa kimitume. Huwezi kutekeleza hilo na kukaa katika dhehebu. Hiyo ni kweli.

200 Sasa, mnaona mambo hayo? Ubatizo wa Roho Mtakatifu, vile karama za Roho, vile vitu ambavyo Mungu huleta . . . Tunda la Roho ni upendo, furaha, uvumilivu, (ee, wasema, "Lakini Ndugu Branham, Mungu ahimidiwe, nina uvumilivu." Yaonekana kama unao. Nilienda kule Ohio hapa muda mchache uliopita, na mtu fulani aliniuliza—aliandika barua hapa na kuniuliza kama mimi hubatiza kwa Jina la Yesu Kristo. Sikusema neno. Walitambua haidhuru, na wahudumu kumi na sita tulioshirikiana nao wakajitenga. Huo ni uvumilivu sivyo!)—uvumilivu, wema, upole, utu wema, saburi, na Roho Mtakatifu. Ona?

201 Ee, Ndugu, Dada, tuko—tuko Kadeshi-barnea. Mnaonja sasa. Usiku uliopita Roho Mtakatifu alitushukia. Aliingia ndani yetu sisi—akaja kama upepo unaovuma. Alikalia juu ya wengi wenu. Leo wahudumu wamekuwa wakizuru manyumbani hapa na pale, kuwekea mikono na kuwaombea wao wanaotafuta Roho Mtakatifu. Usichukue badilisho. Usichukue aina fulani ya kelele. Usichukue aina fulani ya mwamsho. Ngoja mle hadi Mungu amekufinyanga wewe na kukufanya kiumbe kipya, amekufanya mtu mpya. Unamuonja sasa, unamuonja tu, bali acha Hua akuongoze hadi mezani, na—na yule Mwana-kondoo na Hua wakaketi pamoja, na kulishwa daima Neno la Mungu. Maana litadumu wakati hakutakuwako na mbingu na nchi; Neno la Mungu litadumu. Hiyo ni kweli.

202 Tafadhali usidhanie mimi ni mwana mapinduzi. Kama nimekuwa hivyo, sikukusudia kuwa. Kama nime . . . Natumaini nimejibu maswali haya; nimeyajibu, kadiri ninavyofahamu.

203 Na kwa hivyo, katika Waebrania 6, kama mtaona, Paulo akiongea na Waebrania waliosema, "Vema, tutaandamana pamoja nawe umbali huo." Watakuja. Mwaona? Kasema, "Sasa, mme . . . " Hao wajao na wameonja . . .

204 Nilitazama tu jengoni. Kuwaonyesheni ninyi ishara ya Mungu Aliye Hai. Natumai simtazamishi mtu huyu. Nilirudi toka kwa mkutano si muda mrefu uliopita, nikaja hapa na kuwatangazieni ninyi kuwa rafiki mzuri, rafiki msiri wangu, mshiriki katika uwindaji, mtu aliyenikirimia, mtu aliyehudhuria kanisa langu, na amekuwa ndugu yangu; nilimwita Busty. Jina lake lilikuwa Everett Rodgers; aliishi kule Milltown. Wangapi wanakumbuka nikija hapa na kulitangaza? Yeye alikuwa

amelala hapa hospitalini; madaktari walimpasua, wakamfanyia upasuaji, na alikuwa amejaa sana kansa hata wakamshona tu. Kasema, “Yeye atafifia mara moja; katika majuma machache yeye atakuwa amefariki; hayo tu. Yeye atakufa, hivyo tu.”

205 Mwakumbuka jinsi nilivyosimama pale jukwaani, nikamwombea? Nilienda chini kule na kuingia chumbani mle, kitu fulani kikichoma moyoni mwangu. Niliingia chumbani, na mara tu nilipowatoa kila mtu nje ili ni . . . Ndugu Everett alikuwa amelala pale. Na mtakumbuka hili. Nikaingia ndani, nikasema, “Ndugu—Ndugu Busty.” (Nilimwita Busty.)

206 Wakati mwingi uliopita tulipokuwa na mikutano kule kwenye bustani, Wamethodisii wote kule mlimani (Gertie, akiwa mmoja wao), akija kwa siri, akitazama kupitia kwa bandari ya zabibu kuona yale niliyokuwa naenda kusema, vitu kama hivyo, wakiogopa kuwa kanisa Methodisti litawafukuza. Ndiposa, nikaondoka na kuona ono pale, nami nikaona nyama yote imejazwa mkebeni. Nilivua samaki na kuzitia uzi kuziweka—kuzitundika kwenye kiango, nikazitundika kwenye viango. Na nilipotazama . . . Na yote yalikuwa katika ona; ninge—nikaliacha kundi la watu waliosimama chini ya bustani hiyo usiku huo na kukwea hicho kilima hata kwa Ndugu Wright. Nao hata hawangenipata asubuhi iliyofuata. Nikasema, “Hata mmoja wenu . . . ”

207 Nilipokuwa nimesimama pale nikihubiri, hapa ikaja hiyo Nuru; hiyo Nguzo ya Moto ikaning’inia hapa mbele zangu na kuniambia, “Ondoka hapa uende mwituni; nitaongea nawe.” Ilikuwa ni siku ile ile, usiku uliofuata waliponikuta kule kilimani. Na nilikuwa nimekuwa juu kule; nilificha gari langu kwenye magugu, na nilikuwa mlimani nikiomba usiku ule wote na siku nzima iliyofuata. Wengine wao walipanda pale—waliona lile gari na kupanda juu pale . . . Hiyo ilikuwa siku Ndugu Graham Snelling, hapa, alipompokea Roho Mtakatifu na mwito wa kuingia katika huduma.

208 Juu pale kandoni mwa kile kilima ambapo nilikuwa nimelala, kisha yeye—yeye akaniambia mambo mbalimbali ya kutenda na ni ushirika gani tungekuwa nao pamoja. Yeye alitoa ono la kuona hawa samaki waliotundikwa kwenye kiango, kasema, “Hili ni kanisa lako la Milltown.”

Na wanne au watano wao wakaanguka kwa kishindo; nami nikasema, “Huyo ni nani?”

Kasema, “Mmoja wao ni Guy Spencer na mkewe. Yule mwingine ni Spencer mwingine pale, na wengineo.” Naye akaniambia wengineo, wale walioanguka kwa kishindo.

209 Nikawaambia; nikasema, “Hata mmoja wenu asile.” Mimi na mke wangu hata . . . Ilikuwa kabla hatujaoona; naye akaenda nyumbani kukaa usiku mzima na Dada Spencer, mwanamke wa ajabu. Mwanamume wa ajabu, Guy Spencer ni mzuri tu

kama mtu ye yote aliyewahi kuvaa viatu vya ngozi. Naye—naye akaenda kule, kisha Opal akasema, "Sasa tazama . . . " Kwa Meda, yeye alisema, "Sasa, Meda, naamini Ndugu Bill." Yeye alisema, "Lakini Opal ana njaa, inapasa apewe paja la nguruwe na mayai." Kwa hivyo yeye aenda pale, na kumkaangia paja la nguruwe na mayai, na kuketi chini, na kuanza kukiombea chakula hicho, na kuinama mezani, akilia, hangekigusa. Ndipo wakaja kuwinda.

210 Na mle kilimani siku hiyo, yeye aliniambia mimi hasa kile kingetendeka. Yeye alisema, "Hawa wataondoka, kisha hawa wataondoka." Lakini yeye alikuwa na kifurushi kikubwa cha nyama ya mkebe. Akasema, "Weka hiki kwa matumizi ya watu wa Milltown." Na usiku uliopita niliposikia Ndugu Creech . . . Yeye alikuwa ameketi hapo usiku uliopita. Si . . . Ndugu Creech, uko hapa usiku huu? Wakati Ndugu Creech aliponijia, aliponiita, na Dada Creech, akilia; baba yake amelala pale. Kasema, "Ndugu Bill, usimwambie. Yeye anakufa." Kasema, "Ameliwa na kansa; madaktari walimpasua, naye amejaa kansa tupu." Na Will Hall (nanyi nyote mwamkumbuka), wakati daktari yule yule alipompasua, naye alikuwa amejaa kansa . . . Nilianza kwenda kuwinda kuchakulo asubuhi hiyo, nami niliona hizo tofaa zikining'inia chumbani. (Mwakumbuka hadithi hiyo yake?) Ndiye huyu mtu yule anaishi leo. Hiyo imekuwa miaka mingi iliyopita. Yeye na Ndugu Busty walikuwa marafiki.

211 Nami nilienda hospitalini, hospitali mpya (nasahau waiitavyo nje kule katika New Albany)—ile hospitali mpya. Nami nilienda kule kumwona Busty; na nilipoingia chumbani mle, nilisema, "Ndugu Busty."

Yeye alisema, "Ndugu Bill." Akaushika mkono wangu na huko kusalimiana mkononi kwa kale; shujaa wa Vita vya Kwanza vya Dunia, si kusema hili mbele zake, lakini mtu mwenye moyo mzuri tu kama wo wote ule uliowahi kupiga chini ya shati zee la samawati. Yeye akaushika mkono wangu. Nimekuwa nyumbani kwake; nimekula nyumbani kwake; nimelala nyumbani kwake, kama tu kwamba nilikuwa ndugu yake. Watoto wake na kadhalika, sisi tu—tu kama ndugu halisi. Mtu mwema.

212 Naye . . . lakini yeye hakuingia sana kwa Bwana. Yeye . . . Nilimbatiza katika Jina la Yesu Kristo. Lakini siku hiyo huyo mhubiri Mmethodisti aliposema, "Ye yote aliyebatizwa kwa Jina la Yesu Kristo, aondoke chini ya hema langu." Hilo lilikuwa sawa. George Wright na wengineo waliondoka. Alasiri hiyo nikashika njia kwenda kule kubatiza katika Jina Lake Yesu Kristo kwenye Kivuko cha Totten. Kusanyiko lake lote liliingia majini na kubatizwa kwa Jina la Yesu Kristo. Kwa hivyo niliendelea tu. Hilo lilikuwa sawa. Mungu akiwapo upande wako nani aliye juu yako? Hata sijui pale huyo mtu alienda, kipi kilitendeka kwake.

213 Ingawaje, nikaingia mle hospitalini. Ndiye huyo Busty amelazwa pale amejaa kansa, madaktari hata hawenge—hawangefanya lo lote ila kumshona tu alivyokuwa. Busty akaniambia; yeye alisema, "Ndugu Bill, hili lina kusudi fulani. Kitu fulani kilitendeka."

Nikasema, "Naam, Busty." Nilianza kusikia Roho yule kama upepo ukienda kasi ambao nimekuwa nikinena, mwajua, ukiingia.

Akasema...Nilipoingia ndani humo, kulikuwa na upinde wa mvua pembeni mle, ukisimama pembeni mle. Upinde wa mvua ni agano; agano la Mungu. Mungu alifanya agano nami juu ya ule mlima siku hiyo. Niliweka mikono yangu juu ya Ndugu Bustry na kumwombea.

Wale madaktari walisema, "Yeye atafifia kabisa. Atazama. Hakuna la kufanya...Yeye ataaga dunia katika siku chache." Na Busty Rodgers...Hiyo imekuwa majuma mengi sana yaliyopita, na Busty Rodgers anayeketi papa hapa kanisani usiku huu, mwenye afya na mnene kama nilivyowahi kumwona maishani mwangu. Simama, Ndugu Busty. Ndiye huyo. Hebu tumpe Mungu sifa, kila mtu.

Walikuwa wamekusanyika katika chumba cha
orofa, wote wakiomba katika Jina Lake.
Walibatizwa kwa Roho Mtakatifu,
Na nguvu za kuhudumu zikaja.

Sasa, kile Yeye alichowafanyia siku hiyo.
Yeye atakufanyia vivyo hivyo.
Nina furaha tele kuwa naweza kusema, "Mimi
ni mmoja wao."

Mimi ni mmoja wao, mmoja wao;
Nina furaha tele kuwa naweza kusema, "Mimi
ni mmoja wao." (Haleluya!)
Mmoja wao, mimi ni mmoja wao;
Nina furaha tele kuwa naweza kusema, "Mimi
ni mmoja wao."

Ingawa watu hawa hawawezi kudai kuwa
Au kujidai kwa ajili ya sifa za kilimwengu
Wao wote wamepokea Pentekoste yao,
Wakabatizwa kwa Jina la Yesu.
Nao wanatangaza sasa kila mahali,
Nguvu zake zingali vivyo hivyo.
Nina furaha tele kuwa naweza kusema, "Mimi
ni mmoja wao."

Mimi ni mmoja wao, mimi ni mmoja wao;
Nina furaha tele naweza kusema, "Mimi ni
mmoja wao." (Haleluya!)

Mmoja wao, mimi ni mmoja wao;
Nina furaha tele kuwa naweza kusema, "Mimi ni mmoja wao."

Sasa, njoo ndugu yangu, tafuta baraka hii
Itakayousafisha moyo wako toka dhambini,
Itakayoanzisha mlio wa kengele za furaha,
Na itaiwasha nafsi yako.
Ee, inawaka sasa ndani ya moyo wangu,
Ee, Jina Lake litukuzwe
Nina furha tele kuwa naweza kusema, "Mimi ni mmoja wao" (Hebui tuuimbe!)

Ee, mmoja wao, mmoja wao;
Nina furaha tele naweza kusema, "Mimi ni mmoja wao." (Haleluya!)
Mmoja wao, mmoja wao;
Nina furaha tele kuwa naweza kusema, "Mimi ni mmoja wao." (Wangapi ni mmoja wao, inueni mikono yenu? Ee, jamani! Loo, nina furaha jinsi gani mimi ni mmoja wao.)

Mmoja wao mmoja wao; Nina furaha tele kuwa naweza kusema, "Mimi ni minoja wao," (Haleluya!)
Mmoja wao, mmoja wao;,
Nina furaha tele kuwa naweza kusema "Mimi ni mmoja wao."

Walikuwa wamekusanyika katika chumba cha orofa,
Wote wakiomba katika Jina Lake.
Walibatizwa na Roho Mtakatifu,
Ndipo nguvu za utumishi zikaja.
Sasa, kile yeye alichowafanyia siku hiyo,
Yeye atakufanyia vivyo hivyo.
Nina furaha tele kuwa naweza kusema, "Mimi ni mmoja wao."

Ee, mmoja wao, mmoja wao;
Nina furaha tele kuwa naweza kusema, "Mimi ni mmoja wao. "(Haleluya!)
Mmoja wao, mmoja wao;
Nina furaha tele kuwa naweza kusema, "Mimi ni mmoja wao."

Sasa, tunapoimba pambio hiyo tena, nataka kila mmoja wenu ageuke na kusalimiana kwa mikono na mtu mwingine aliye kando yako na kusema, "Je, u mmoja wao?" Ona? Vema.

Ee, mmoja wao (Najua ndivyo ulivyo, Mugu. . .? Najua andivyo ulivyo, Ndugu. . .?. . .) [Ndugu Branham asalimiana

kwa mikono na wale walio karibu naye—
Mh.] . . . mmoja wao.

Ee mmoja wao mmoja wao;
Nina furaha tele naweza kusema "Mimi ni
mmoja wao."

214 Ee, hamna furaha kuwa ninyi ni mmoja wao. Wangapi wangependa kuwa mmoja, inueni mikono yenu? Vema. Sasa, nitawaimbieni huu:

Basi njoo ndugu yangu, tafuta baraka hii
Itakayokusafisha moyo wako toka dhambini,
Itakayoanzisha mlio wa kengele za furaha.
Na itaiwasha nafsi yako.
Ee, inawaka sasa ndani ya moyo wangu,
Ee, Jina Lake litukuzwe.
Nina furaha tele kuwa naweza kusema kuwa,
"Mimi ni mmoja wao."

Ee, mmoja wao, mmoja wao;
Nina furaha tele kuwa naweza kusema, "Mimi
ni
mmoja wao." (Haleluya!)
Mmoja wao, mimi ni mmoja wao,
Nina furaha tele kuwa naweza kusema, "Mimi
ni mmoja wao."

215 Kumbuka aliyosema maskini msichana yule, "Petro si wewe ni mmoja wao?" Nina furaha tele, nawe je? Mwajua, Petro alisema kwenye ile siku ya Pentekoste, "Jambo hili ni lile!" Sasa, mimi kila mara nimekuwa nikisema, "Kama jambo hili ni lile, nina furaha nimelipata hili, nikingoja lile lije." Naam. Ninafurahia hili.

Kwa kuwa ni mmoja wao, mimi ni mmoja wao;
Nina furaha tele kuwa naweza kusema, "Mimi
ni mmoja wao."
Ee, mmoja wao, mmoja wao;
Nina furaha tele kuwa naweza kusema, "Mimi
ni mmoja wao."

216 Ee, si ajabu hii, kuketi pamoja katika ulimwengu wa roho katika Kristo Yesu, tukishiriki katika Roho, kushiriki kwa Neno, kunena juu ya mambo mazuri yajayo. Ni vizuri sana. Nina furaha tele kujua hayo, nanyi je? Je, hamfurahi kuwa Wakristo? Je, mna furaha dhambi zenu ziko chini ya Damu? Yeye yuaja hivi karibuni, nasi tutaenda pamoja Naye. Basi wazia, uzee wote utatuondokea; magonjwa yote, kuungua kwote, maisha haya yote yafayo yatabadilika. Jamani. Naweza kuwaza juu ya ndugu wapendwa wazee waliosimama hapa. Nakumbuka . . . Wangapi mwamkumbuka Rabi Lawson? Lo, wengi wenu. Naweza kumwona akiuweka ule mkongojo papa hapa. Nami ningekuwa nimeketi nyuma kule. Yeye angeuimba

ule wimbo mdogo . . . (Hebu kidogo Teddy, Ndugu.) Nitajaribu—kuona kama ningepata sauti yake. Sijui.

> Kesho yenye furaha yaningoja,
> Ambapo malango ya lulu yatafunguliwa wazi,
> Na nivukapo pazia hili la huzuni,
> Nitapumzika ng'ambo ya pili.
>
> Siku moja wasikofika viumbe wafao,
> Siku moja, Mungu pekee ajua wapi na ni lini,
> Gurudumu la maisha yafayo litatulia,
> Ndipo nitaenda kuishi kwenye mlima wa Sayuni.

217 Haya magurudumu madogo yanayozunguka ndani yetu—kuona, kuonja, kuguswa, kunusia, na kusikia, hizi hisi ndogo na gurudumu linalozunguka katika haya maisha yanayokufa, wakati moja yatatulia. Kisha mimi, mwenyewe, na wewe, tutaenda kuishi kwenye mlima wa Sayuni. Ee, napenda hilo, nanyi je? Jueni tuna hiyo dhamana yenye heri. Vema. Wangapi wajua wimbo wetu wa kale wa ubatizo? Sasa, tutaugeuza huo. Hebu tuimbe wimbo wetu wa kumalizia:

> Peleka Jina la Yesu
> Po pote uendako,
> Litafurahisha moyo;
> Peleka uendako.

Peleka Jina la Yesu. Hebu fanyeni hivyo, mnapoondoka. Vema pamoja sasa. Msisahau, saa 2 asubuhi kadi za wanaohitaji kuombewa zitatolewa mkutanoni. Mkutano utaanza saa tatu na nusu. Nitahubiri saa nne. Ibada ya kuombea wagonjwa itaanza saa tano.

Kesho alasiri—kesho jioni itakuwa ni ujumbe wa kiinjilisti hapa maskanini. Na kesho usiku, ninyi nyote ambao mmetubu dhambi zenu na hamjawahi kubatizwa, kutakuwako—bwawa litafungiliwa; tutawabatiza watu kwa Jina la Bwana Yesu Kristo.

Kila mtu pamoja sasa, tunapoimba kwa sauti yetu yote. Ndugu Busty, hujui nimefurahi jinsi gani na kumtolea Mungu shukrani. Mwajua, yeye alienda kwa daktari. Na waliniambia daktari yule alimtazama, na hakujua la kuwazia. Yeye hakuamini ni mtu yule yule. Ee, si siri yale Mungu awezayo kufanya. Sivyo? Vema.

> Peleka Jina (litamke!) la Yesu,
> Po pote uendako;
> Litafurahisha moyo;
> Peleka uendako.

Thamani, (Thamani!) na tamu!
Ni Jina Lake Yesu
Thamani (Thamani!) na tamu!
Ni Jina Lake Yesu

Vema. Nairudisha sasa ibada kwa mchungaji. Yeye atakuwa na maneno machache, au anene kisha mtu mwingine atuachie tuondoke, cho chote kilicho niani mwake.

Mwenendo, Utaratibu Mafundisho ya Kanisa, Kitabu Cha Kwanza
(Conduct, Order And Doctrine Of The Church, Volume One)

Jumbe hiza za Ndugu William Marrion Branham, ziliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali zilitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings. Ilichapishwa tena katika mwaka wa 2013.

SWAHILI

©2009 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org